## **Chongolo** ataka subira suala la uwekezaji bandari



UKURASA 3

## **Watu** watatu wahofiwa kufa maji ajali boti

UKURASA 5


MAISHA
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili
MAISHA NI NYUMBA
MAKANDE YA NYAMA
Wajua zulia huongeza mvuto kwenye nyumba?
KATUNIKA
KOMESHA MBA

UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 23, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581380

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Mume adaiwa kuua mke, ndugu kisa wivu mapenzi

UKURASA 2



Salehe Ally anayedaiwa kufanya mauaji hayo



Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, ACP Gideon Msuya, akiwaonyesha waandishi wa habari, gari aina ya Toyota Hilux Double Cabin lenye namba za usajili T476 DZL, lililogonga kundi la vijana wa klabu ya mazoezi ya Aden Hotel na kusababisha vifo vya watu sita na majeruhi 16, jijini Mwanza jana. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Ajali ilivyoua sita, kujeruhi 16 'jogging'

UKURASA 3

UKURASA WA 4

### SERIKALI YATAFUTA MWAROBAINI MATUMIZI HOLELA YA DAWA ZA P2

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali inatafuta mbinu ya kuzuia matumizi holela ya dawa za dharura za kuzuia mimba, maarufu...

## Mpango afichua mbinu viongozi kujipatia rushwa

UK. 2

**MICHEZO** **SKUDU, MKUDE WAITEKA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akimsikiliza Mkurugenzi wa Kitengo cha Uangalizi wa utajiri wa asili na maliasili za nchi kwa Wizara ya Katiba na Sheria, SACP Neema Mwanga (kulia), alipotembelea banda la wizara hiyo, kabla ya kuzindua kampeni ya Kitaifa ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia katika Uwanja wa Majimaji, mjini Songea mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mpango aibua mbinu za vigogo kujipatia rushwa

**Na Waandishi Wetu,** SONGEA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameibua mbinu za viongozi na matajiri kutoka nhi jirani kujineemesha na rushwa na migogoro inayosababishwa na wakulima na wafugaji.

Amesema baadhi ya viongozi wametengeneza mbinu za kujipatia hadi Sh. Milioni tano ili kupitisha malori yanayobeba mifugo.

Kutokana na kuwepo kwa mbinu hizo, ameagiza vyombo vya ulinzi na usalama kushughulikia migogoro ya wakulima na kupambana na viongozi wenye tabia hiyo.

Aidha, amelitaka Jeshi la Polisi kuwabaini viongozi hao pamoja na askari polisi wanaoruhusu na kupitisha malori yaliyobeba mifugo na kujipatia Sh. 100,000 hadi 120,000 kwa kila ng'ombe na kwa kila roli linalopitishwa, wamekuwa wakipata hadi Sh. milioni tano.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana wakati akizindua kampeni ya kitaifa ya msaada wa kisheria inayoitwa 'Mama Samia Legal Aid 2023/24' iliyofanyika uwanja wa Majimaji mjini hapa.

Kiongozi huyo alisema ana taarifa kuwa kutokana na migogoro ya wakulima na wafugaji, kuna migogoro ya ardhi mingi inachangiwa na baadhi ya viongozi pamoja na askari polisi ambao wamekuwa wakila rushwa kwa kupitisha mifugo kinyume cha sheria za nchi licha ya serikali kupiga marufuku uingizaji wa mifugo holela mkoani hapa.

Dk. Mpango aliagiza viongozi hao na askari wanaohusika wachukuliwe hatua na kama watashindwa kufanya hivyo, apewe majina yao atawashughulikia.

Alisema kumekuwapo na vitendo vya ukatili ambavyo vinaongezeka kupitia migogoro ya ardhi kwa wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kufanya uharibifu mkubwa, hivyo amevitaka vyombo vya usalama kuwachukulia hatua watu wote wanaohusika.

"Ninayo taarifa ya baadhi ya viongozi wa mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na baadhi ya matajiri kuingiza mifugo kinyemela.

Pia wapo baadhi ya askari polisi nao wanapitisha malori yaliyosheheni ng'ombe na kila ng'ombe wanamchaji Sh. 100,000 hadi Sh. 120,000 kwa roli moja. Wanapata hadi Sh. milioni tano, hali ambayo ni hatari kwa usalama wa nchi," alisema Dk. Mpango

Alisema kati ya Januari na Desemba 2022, vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeongezeka na kwamba zaidi ya matukio 2,000 yameripotiwa na kati ya hayo ubakaji ni zaidi ya 6,000, ulawiti 5,000 na mimba za utotoni 1,000.

Dk. Mpango amevitaka vyombo vya dola kuwachukulia hatua watu wote wanaohusika ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.

Aliwaagiza viongozi kuanzia ngazi ya kata, watendaji na wenyeviti wa serikali za mitaa na vijiji kutoa elimu kwa jamii kuhusu ukatili wa kijinsia.

Dk. Mpango pia aliwataka watu wenye uhitaji wa msaada wa kisheria kutumia nafasi hiyo kikamilifu ili waweze kupata haki zao.

"Wananchi wapate huduma kwa wakati kupitia kampeni hii ili kuongeza uelewa kuhusu misingi ya haki na upatikanaji wa haki, kuboresha upatikanaji wa haki hasa kwa watu wasio na uwezo, hasa wanawake, watu wenye ulemavu, watoto na watu wa makundi mengine," alisema.

Aidha, aliiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuongeza kasi ya upimaji na upangaji wa miji ikiwa ni pamoja na kurasimisha makazi ya wananchi kwa kuzingatia sheria

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, ambaye ni Mbunge wa Songea Mjini, alisema mkakati wa kampeni ya Mama Samia unalenga kuongeza uelewa wa msaada wa elimu kwa wananchi hasa wanyonge na wanaotoka sehemu za pembezoni na tayari imesaidia mahabusu.

Alisema tangu kuanza kwa kampeni hiyo, Ruvuma ni mkoa wa nne ukitanguliwa na Dodoma, Manyara na Shinyanga na lengo ni kufikia mikoa mbalimbali.

Ndumbaro alisema halmashauri 21 zimepitiwa na mkakati unahusisha pia taasisi mbalimbali zinazojishughulisha na elimu ya msaada wa kisheria na tayari imeshatatua zaidi ya migogoro 2,000 na wananchi wameandika wosia na imetoa haki na usawa.

Dk. Ndumbaru aliwaonya wananchi wenye tabia ya kutoa lugha za kudhalilisha viongozi kwa kuwatukana kwenye mitandao ya kijamii kuacha tabia hizo na watumie fursa hiyo kutoa maoni yenye staha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dk. Selemani Jaffo, alitumia fursa hiyo kuwakumbusha wananchi kutunza mazingira.

"Muda si mrefu kuanzia Septemba utasikia Longido wanyama wakifa kwa kukosa maji kwa sababu ya ukame, hivyo Watanzania tujitahidi kutunza mazingira ili kuokoa uoto wa asili," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Jenister Mhagama, alimshukuru Rais Samia Suluhu kwa kupeleka maendeleo mkoani Ruvuma ikiwamo miradi ya kimkakati kama reli kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay.

Pia alimshukuru Rais Samia kwa kujenga miundombinu ya barabara ya Namtumbo- Mahenge- Morogoro kwa kiwango cha lami.

**Iimeandaliwa na Gideon Mwakanosya na Ibrahim Joseph (SONGEA)**


KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NA. 36 YA MWAKA 2023

INNOCENT BENEDICT MBERESERO.....................MDAI

DHIDI YA

1. FRANK THOMAS NYILIKA.........MDAIWA
2. VGK CO. LTD.....................MDAIWA
3. THE JUBILEE INSURANCE COMPANY OF TANZANIA LTD............MDAIWA

Kwa: FRANK THOMAS NYILIKA – DAR ES SALAAM – Simu Na. 0658 606355

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la maombi ya madai dhidi yako; shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya madai zinazopatikana katika Mahakama hii kupitia wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria, siku ya tarehe **22/8/2023** saa tatu (3:00) kamili asubuhi mbele ya **Mhe. Jaji M.K. Pomo,** kujibu maombi hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika usikilizaji wa shauri hili.

**ANGALIZO:**
Kama usipohudhuria siku hiyo iliyotajwa juu, na Mahakama ikithibitisha kama umepokea taarifa ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamriwa bila uwepo wako.

**HATI** hii imetolewa kwa **AMRI** yangu na **CHAPA** ya Mahakama leo hii tarehe 19/7/2023.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM



IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOROGORO DISTRICT REGISTRY
AT MOROGORO

LAND APPEAL NO.70 OF 2023

NDESHUKURWA ABEL SUMARI.............APPELLANT

VERSUS

CYREKA EAST AFRICA DEVELOPMENT CO.LTD............RESPONDENT

NOTICE TO APPEAR
SUBSTITUTED SERVICE

(Made under order V rule 16 of the Civil procedure code, cap.33 R. E2019)

TO: CYREKA EAST AFRICA DEVELOPMENT CO.LIMITED

**TAKE NOTICE** that the above named Appellant has instituted an appeal against you and the same is fixed for MENTION on 31st day July, 2023 at 09:30 A.M, before Hon.M.J.CHABA,J. in the HighCourt of Tanzania at Morogoro.
You are thus required to appear in person or through your advocate or dully authorized agent without fail.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on the afore mentioned date and time,the Court shall proceed to hear and determine the case in your absence.
**GIVEN under my HAND and SEAL** of this COURT this 12nd July,2023.

DEPUTY REGISTRAR
MOROGORO


## Mume adaiwa kuua mke, ndugu kisa wivu mapenzi

**Na Steven William,** MUHEZA

WANAWAKE wawili wa familia moja wakazi wa kijiji cha Mkanyageni, Muheza mkoani Tanga, wameuawa kwa kukatwakatwa na panga kwa madai ya wivu wa mapenzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Henry Mwaibambe, alisema tukio hilo lilitokea juzi baada ya Ally kumtuhumu mke wake, Mwanahawa Khatib kuwa anamsaliti katika ndoa yao.

Mbali na kumuua mke wake huyo, Kamanda Mwaibambe alisema Ally alimuua pia Sauda Sufiani ambaye ni ndugu na Mwanahawa.

Alisema baada ya kutekeleza mauaji hayo akiwa porini, mtuhumiwa alikimbilia kusikojulikana na Jeshi la Polisi mkoani Tanga linamsaka ili hatua za kisheria dhidi yake zichukuliwe.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mkanyageni, Athumani Azacha, akizungumzia tukio hilo, alisema mtuhumiwa alikuwa na wake wawili, mke mkubwa na mke mdogo.

"Juzi majira ya saa 12:00 asubuhi, mtuhumiwa alitoka kwa mke mkubwa akaenda kwa mke mdogo ambaye ni Mwanahawa wakaondoka wakiwa watatu akiwamo Sauda kwenda kuchukua kuni porini.

"Ilipofika majira ya saa 2:00 asubuhi mtuhumiwa alirudi nyumbani akiwa peke yake na alipoulizwa kuhusu wenzake wawili waliko, yaani Mwanahawa na Sauda. Baada ya kuulizwa hivyo mtuhumiwa alijibu kuwa amewaacha shambani wakichuma mboga na kwamba watarudi baadaye.

Mwenyekiti huyo alisema watu walisubiri nyumbani hapo na ilipofika majira ya saa 4:00 asubuhi walipata wasiwasi na kuingia porini kuwasaka bila mafanikio.

Alisema kundi la tatu liliingia tena msituni majira ya saa 10:00 jioni ndipo walipomkuta Mwanahawa amefariki dunia kwa kukatwa na mapanga na wakati huo Sauda hakuonekana.

Azacha alisema kundi hilo lilipomtafuta bila mafanikio na waliporudi nyumbani mtuhumiwa alipiga simu akiwa mafichoni, akieleza kuwa Sauda naye ameuawa na maiti yake iko chini ya mkorosho na kuwataka waende kuichukua.

Mwenyekiti huyo alisema wananchi kwa kushirikiana na askari polisi wa kituo kidogo cha Mkanyageni, walifika eneo la tukio na kukuta mwili wa pili. Miili ya marehemu imehifadhiwa Hospitali ya Teule ya Wilaya ya Muheza.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mkanyageni, Lusi Mrai, na Diwani wa Ngomeni, Bakari Mhando, kwa nyakati tofauti walisema mauaji hayo ya watu wa familia moja yameibua taharuki kubwa kijijini hapo.

Ndugu wa familia hiyo, Mwanavita Abdallah, mama wa marehemu Mwanahawa na Adam Hatibu ambaye ni mume wa marehemu, Sauda Sufiani na Hatibu Luku kwa nyakati tofauti walisema kitendo hicho kimeiachia familia simanzi.

HABARI KITAIFA

## Chongolo ataka subira uwekezaji bandari

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka watanzania kuwa na subira kwenye suala la uwekezaji katika bandari ya Dar es Salaam kwa kuwa matokeo yenye tija yataonekana baadaye.

Pia amesema upotoshwaji katika suala hilo ni vita ya kiuchumi ambayo haiwezi kushikwa wala kuiona kwa macho na Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye fursa nyingi za kiuchumi, hivyo ni vyema kuyapima maneno hayo.

Alisema hayo jana katika mkutano wa hadhara wa kutoa elimu ya makubaliano ya serikali ya Tanzania na Dubai kuhusu uendeshaji wa bandari ulioshirikisha wananchi kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

"Nasi tunapenda kupendwa na wananchi, hatuwezi kufanya jambo lisilo na tija kwa taifa. Tuvute subira matokeo yake tutayaona na tuachane na upotoshaji unaoendelea. Ni vizuri kila mmoja akatambua hii ni vita ya kiuchumi hakuna anayetutakia jema la nchi yetu," alisema.

Pia alisema kutokana na miradi mbalimbali inayoendelea nchini, kunahitajika fedha nyingi na moja ya njia za kupata fedha hizo ni kwenye uwekezaji wa bandari.

"Hata kwenye suala la utengenezaji wa filamu ya The Royal Tour, watu wengi walibeza lakini leo tunaona matunda yake. Kufurika kwa watalii kwenye vivutuo vyetu mbalimbali na watu wanapata matunda ya filamu hii. Hatumkumbuki wala kumshukuru tena Rais Samia Suluhu Hassan na matokeo yake,' alisema.

Chongolo alikemea baadhi ya watu wanaomtukana Rais badala yake amewataka waje na hoja za kusaidia serikali kuboresha makubaliano hayo kwa faida ya taifa. "Tunakaribisha maoni ya watu juu ya suala hili lakini yote ya dharau, kebehi na matusi hatutayapokea na badala yake tutasonga mbele na mwisho wa siku watakuja kuishukuru serikali kwa maendeleo makubwa tutakayoyafikia," alisisitiza.

Alisema kazi ya kuongoza nchi si lelemama inataka mtu kukaa imara na kusimamia mipango anayoiamini bila kuyumba au kuingia kwenye mitego ya wasiolitakia mema taifa.

"Ukiona adui yako anakupigia makofi katika jambo lako, achana nalo halina tija. Ukiona adui anakupigia kelele kaza buti nenda mbele kwa sababu wanajua ukilitekeleza kwa kiwango hicho watakosa kupata dhamana mwaka 2025 nasi tunapenda kupendwa.

"Mpango unaoendelea sasa wa uwekezaji ni utekelezaji wa Ilani ya CCM. Wapo wanaohangaika kutupiga breki ili tusiendelee na utekelezaji huu na baadhi yetu wanaingia katika mtego wa kuanza kubishana. Mtu asiyekupenda hawezi kukushauri jambo lenye tija," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema a wekezaji wa bandari ya Dar es Salaam, utafanywa na wafanyabiashara, wakati serikali ikibaki katika jukumu lake la msingi la ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi.

"Kuwepo kwa bandari ni upendeleo wa kijiografia tuliobahatika kuwa na bandari. Si nchi zote zimebarikiwa lakini ni jukumu letu kutengeneza miundombinu ili ziwe na faida za kiuchumi na tumekuwa tukizitengeneza mara kwa mara, lakini bado ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam ni mdogo.

"Tunahitaji uwekezaji mkubwa pamoja na kuboresha utendaji, ili tupanue magati yetu, kwa ajili ya kuhudumia mizigo mingi zaidi," alisema.

Prof.Kitila alisema katika uwekezaji huo, mwekezaji amepewa eneo la hekta 7.5 sawa na asilimia nane ya eneo la bandari lenye ukubwa wa hekta 667.

# Ajali ilivyoua sita, kujeruhi watu 16 wakiwa 'jogging'

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATU sita waliokuwa wakifanya mazoezi, maarufu kama 'jogging' katika eneo la Sabasaba, barabara ya Kiseke, Wilaya ya Ilemela mkoani hapa, wamefariki dunia na wengine 16 kujeruhiwa baada ya gari kuacha njia na kuwagonga.

Kundi hilo la mazoezi maarufu kwa jina la Aden Hotel wakati likiendelea na mazoezi majira ya saa 12:30 asubuhi maeneo hayo ndipo gari lilipoacha njia na kwenda kuwagonga.

Katika tukio hilo, watu sita walifariki dunia papo hapo na wanne kati ya 16, hali zao ni mbaya. Baadhi wanapatiwa matibabu katika Hospitali za Rufani Mkoa Sekou Toure na wengine ya Rufani Kanda Bugando.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Gideon Msuya, alilitaja gari lililosababisha vifo hivyo ni Toyota Hilux Double Cabin lenye namba za usajili T476 DZL na dereva wake anaendelea kusakwa baada ya kukimbia.

Alisema baada ya dereva huyo kusababisha ajali hiyo, aliendelea na safari na kwenda kulitelekeza gari hilo kwenye kituo cha mafuta.

Msuya alisema waliofariki dunia wote ni wanaume kutoka klabu ya mazoezi ya Aden Hotel ambao ni Mkongolo Mayanda, Peter Fredrick, Shadrack Safari, Seleman Daud, Hamis Waziri na Aman Matinde.

"Waendesha vyombo vya moto wanatakiwa kutambua kuwa siku ya Jumamosi watu huitumia kufanya mazoezi, hivyo wanatakiwa kuchukua tahadhari wakati wote wakiwa barabarani," alisema ACP Msuya.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, kupitia ujumbe wake wa pole, alisema miili imehifadhiwa katika Hospitali ya Sekou Toure na majeruhi wanne wenye hali mbaya wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Bugando na wengine 10 hospitali ya Sekou Toure.

Alisema taratibu za kukabidhi miili kwa ndugu wa marehemu zinaendelea kuratibiwa.

"Nitoe pole kwa familia zilizopoteza wapendwa wao na tuendelee kuwaweka kwenye maombi majeruhi wote wapate uponyaji wa haraka na waruhusiwe warudi nyumbani kuendelea na majukumu yao," alisema.

Mwandishi wa habari hii akizungumza na mmoja wa majeruhi aliyelazwa katika Hospitali ya Sekou Toure, Peter Andrew, ambaye ni Meneja wa Hoteli ya Aden Palace, alisema kila Jumamosi amekuwa akifanya mazoezi hayo ambayo hufanyika kuanzia saa kumi na mbili asubuhi.

"Nilisikia tu kishindo cha kugongwa kwa nyuma nikapoteza fahamu. Baada ya muda kidogo, nilishtuka na kuwakuta wenzangu wengi wamelala nikagundua kuwa wako waliovunjika na wengine wakiwa wamefariki dunia na baada ya hapo tuliletwa hospitalini,"alisimulia.

Shuhuda wa ajali hiyo, John Mathew, ambaye ni dereva bajaji alisema gari hilo lilitokea nyuma yake likiwa kwenye mwendo kasi na lilizuiwa na mnyanyua vibendera wa mazoezi hayo hizo ambaye baadaye liliruhusiwa.

"Baada ya kuruhusiwa inaonekana dereva hakuelewa ishara hizo ndipo alipowapelekea gari na kuanza kuwagonga (wanaofanya mazoezi).

Na baada ya kuwagonga hakusimama akaendelea na mwendo kasi, lakini gari lilifika mbele likazimika, wakashuka (baadhi ya watu) kulisukuma na kulipeleka kwenye kituo cha mafuta kisha wakakimbia, sikujua walipoelekea tena,"alisimulia Mathew.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Sekou Toure, Dk. Bahati Msaki, alisema majeruhi waliopokewa hospitalini hapo ni 16 wakiwamo wanawake wawili na wanaume 14.

Alisema wanane walipelekwa Bugando na saba wamelazwa hospitali hapo na mmoja kati yao ameruhusiwa.

"Tumepokea miili mitano ya watu ambao walifariki dunia katika eneo la tukio na mmoja alifariki dunia akiwa hospitalini kwetu baada ya kufikishwa akiwa na hali mbaya," alisema.


## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LIMITED** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi/Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | RAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MASIKA JOHN MASSAWE | MASIKA JOHN MASSAWE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BOMBANI STREET CHEKERENI WARD(BONITE) IN MOSHI | 12/08/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LIMITED |
| 2. | OMARI H. NGOZWA | OMARI H. NGOZWA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | KIJIJI CHA MABOGINI MOSHI | 12/08/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilyopo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe yamnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LIMITED**
**P.O.BOX 12943**
**ARUSHA**
**TEL:0752 632 033, 06 28 5 12 033**
**Eamail: mangwembe@gmail.com**

217511102




Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Uratibu wa Udahili na Menejimenti ya Data wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Dk. Kokuberwa Katunzi (kushoto), alipotembelea banda la TCU wakati wa kufunga Maonyesho ya 18 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yatafuta mwarobaini matumizi holela ya dawa za P2

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali inatafuta mbinu ya kuzuia matumizi holela ya dawa za dharura za kuzuia mimba, maarufu kama P2 na kwamba haitazuia uuzaji wake.

Waziri Ummy ameyasema hayo jana wakati akizindua utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kuhusu namna vyombo vya habari vinavyoripoti habari za Haki ya Afya ya Uzazi (SRHR) kwa wanawake wa mijini na vijijini.

"Lengo letu lilikuwa zuri kuwezesha upatikanaji wa dawa hizo na huduma kwa ajili ya afya ya uzazi, yaani mtu amebakwa au mtu amepewa ujauzito na mzazi wake, apate urahisi wa kupata huduma hii kwani ni sehemu ya uzazi wa mpango wa dharura," alisema.

Waziri Ummy alisema lengo halikuwa baya bali dawa hizo zimekuwa zikitumika holela na tayari alishamwelekeza Mfamasia Mkuu wa Serikali na timu yake walifanyie kazi.

"Hatutaki kuzuia upatikanaji wake kwa sababu zinasaidia. Kuna mtu amebakwa na mzazi au jirani ndani ya ule muda aweze kupatiwa, nitalifanyia kazi. Sisi kama serikali tutajielekeza katika kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya P2," alisisitiza.

Waziri Ummy alionya matumizi ya dawa hizo kiholela akisema zinavuruga homoni.

"Sasa wewe unatumia kila siku, unaweza kuingia kwenye tatizo la kupata saratani, ugumba hawaelewi ila madhara yake ni makubwa sana,"alisisitiza.

Hata hivyo, Waziri huyo alisema katika kudhibiti dawa hizo kwao itawapa shida kwa sababu zinasaidia pale mtu anapopata matatizo, hivyo watajikita zaidi katika kutoa taarifa sahihi.

"Kama kuna uwezo wa kudhibiti tutadhibiti labda asiruhusiwe mtu mwenye umri chini ya miaka fulani. Ukisema mtu mpaka aende kwa daktari aandikiwe cheti, tutakwenda kuweka kama kikwazo cha upatikanaji wa huduma hizi," alisema.

Waziri Ummy alisema watajikita kutoa elimu wa kwa jamii hususani wasichana kuhusu matumizi sahihi ili kuepuka madhara yake ikiwamo kuweka mabango katika maduka ya dawa kama walivyofanikiwa kwenye ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB).

Kuhusu utafiti wa TAMWA, alisema utasaidia kushirikiana kwa pamoja katika masuala ya afya ya uzazi ya mama na mtoto.

"Waandishi wa habari mtatusaidia kwa nini Mbeya matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango ni asilimia 58, Njombe asilimia 64, Kilimanjaro asilimia 63 na Iringa asilimia 55 mnaweza kupata taarifa zaidi," alisema.

Alisema changamoto kwa sasa imebaki kwenye vifo vya watoto wenye umri wa siku moja hadi siku 28 ambavyo wanaendelea kupambana.

Pia alitaja eneo lingine ambalo wanakwenda kulipa kipaumbe ni la watoto njiti kwa kutoa vifaa tiba na kuvisambaza nchi nzima ili kuhakikisha kila hospitali ya Wilaya inakuwa navyo.

"Utafiti huu wa TAMWA umekuja wakati sahihi, kuna haja ya kuboresha upatikanaji wa taarifa na huduma kuhusu afya ya uzazi kwa wanawake na wanaume wa mijini na vijijini," alisema.

Kuhusu afya ya uzazi kwa vijana Waziri huyo alisema kuna baadhi wanaitumia vibaya na kutaka waendelee kupatiwa elimu ili waweze kujitambua na kutojiingiza kwenye mambo ambayo ni kinyume na mila na desturi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alisema utafiti huo umekusanya maudhui kutoka kwenye maandiko ya wanasayansi, mahojiano kutoka kwa wanahabari, wahariri na wadau wengine wa habari.

Alisema matokeo ya utafiti yanaonyesha kuna uchapishwaji mdogo wa maudhui ya Haki ya Afya ya Uzazi (SRHR), hakuna uchapishaji wa habari za kina za utendaji, kampeni za kiafya na uchunguzi kuhusu SRHR.

Reuben alisema wameona haja ya wataalamu wa afya, wanasayansi, watafiti kuwa na mtazamo mmoja ili kuripotiwa vyema na kwa ufanisi masuala ya haki za afya ya uzazi.

"Kutokana na ombwe hilo, TAMWA tumeona kuna haja ya kuwa na sera ya afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana katika vyombo vya habari, ili kuongeza wigo kwa kuripoti habari hizo,"alisema.

Alisema kuwapo kwa sera ya matumizi sahihi ya dawa za uzazi wa mpango ikiwamo P2 na mwongozo na uratibu sahihi utakaodhibiti matumizi holela ya dawa hizo na mabadiliko ya sheria ya ndoa.

## Uchafu maji wasitisha huduma ya uji shuleni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Bulambilia wilayani Shinyanga, Pius James, ameeleza namna walivyositisha huduma kwa wanafunzi ya unywaji wa uji shuleni kutokana na maji wanayotumia kupikia kuwa machafu.

James aliyasema hayo juzi mbele ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja, aliyefika shuleni hapo kuangalia huduma ya majisafi. Alisema kabla ya kupeleka huduma ya maji safi na salama, walilazimika kusitisha utoaji wa uji kwa wanafunzi.

Aliishuku serikali pamoja na wadau wa maendeleo ambao ni Life Water kwa kuwapelekea huduma ya majisafi na salama.

"Huwa tuna utaratibu wa kutoa uji kwa wanafunzi na maji ambayo yanatumika kupikia wanafunzi wamekuwa wakija nayo. Kutokana ukosefu wa majisafi na salama eneo hili, maji ambayo yalikuwa yanaletwa yalikuwa machafu zaidi ndipo tukaona tusitishe huduma hiyo ili kuokoa afya za wanafunzi,"alisema James.

Alisema kutokana na huduma ya maji safi na salama kupatikana shuleni hapo kwa sasa, wataendelea kutoa uji kwa watoto kama ilivyokuwa awali kwa kuwa hupunguza njaa na wanafunzi kuacha utoro.

Mwanafunzi wa darasa la saba shuleni hapo, Flora Mussa, alisema upatikanaji wa maji umewaondolea adha ya kubeba maji kila siku kutoka nyumbani na hatua hiyo itaimarisha usafi kwenye vyoo vya shule.

Luhemeja akiwa shuleni hapo, aliziagiza mamlaka zote za maji na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) zinapotekeleza miradi ya maji zihakikishe zinapeleka huduma hiyo pia katika taasisi zote za serikali zikiwamo shule, vituo vya afya na zahanati.

Pia, alizitaka mamlaka hizo kutoa elimu kwa wananchi kuvuta mabomba ya maji majumbani mwao ili kutekeleza adhma ya kumtua ndoo kichwani mwanamke na kuacha kuendelea kuchota kwenye vituo.

Katika hatua nyingine, akiwa katika mradi wa maji wa Ziwa Victoria, Tinde wilayani Shinyanga, aliiagiza Mamkala ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), kuhakikisha Mkandarasi ambaye anatekeleza kazi ya kusambaza nishati hiyo kwa wananchi katika vijiji 22 ahakikishe anaanza kazi hiyo hadi kufikia Agosti.

Mbunge wa Solwa, Ahmed Salum, aliipongeza serikali kwa kutekeleza miradi ya maji kwa wananchi hasa wa maeneo ya vijijini.

Alisema awali walikuwa wakikabiliwa na hali mbaya lakini sasa wengi wanapata huduma hiyo zikiwamo na taasisi za serikali na kubaki maeneo machache.

## HABARI KITAIFA

# Watatu wahofia kufa maji kwa ajali ya boti

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WATU watatu kati ya 26 wanasadikiwa kufa maji katika ajali ya boti iliyozama kilometa 10 baada ya kuanza safari ikitokea katika Kisiwa cha Kerebe, katika Ziwa Victoria, Muleba mkoani Kagera kuelekea Bukoba.

Akizungumza kwa mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kagera, Zabron Murumha, alisema walipokea taarifa za ajali hiyo majira ya asubuhi na vijana wa jeshi hilo walioko katika wilaya ya Muleba walifika kutoa msaada.

Alisema na jitihada za kuwatafuta ambao hawajapatikana zinaendelea.

Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Abel Nyamahanga, alisema ajali hiyo ilitokea jana saa 1:00 asubuhi baada ya injini mbili za boti hiyo kuzima na kusababisha kuyumba kutokana na hali ya hewa kuwa ya upepo, hivyo kugonga jiwe.

Alisema kwa mujibu wa kitabu cha abiria, boti hiyo ilikuwa na abiria 26 na kati ya hao, wanne ndio walioumia na kupelekwa hospitalini kwa matibabu na 21 walitoka bila kuwa na majeraha na mmoja akiwa hajapatikana huku kukiwa na taarifa kutoka eneo la tukio kuwa wasioonekana ni watu watatu.

"Wasiwasi ulikuwa ni mtu mmoja, lakini inaelezwa kuwa ni watatu ambao hadi sasa hawajapatikana," alisema.

Nyamahanga alisema juhudi za kutafuta ambao wanasadikiwa kuwamo kwenye boti hiyo zinaendelea kufanywa na kikosi cha zimamoto na wananchi.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano Vivo Energy Tanzania, Grace Kijo (kushoto), akiwa na mshindi wa bodaboda wa promosheni ya "Jaza Ushinde Tena na Engen" kutoka Morogoro, Finias Boniface aliyejishindia zawadi hiyo baada ya kushiriki kujaza mafuta kwenye vituo vya Engen na kuingia kwenye droo hiyo, baada ya kukabidhiwa zawadi yake, mjini Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 500/- kujenga kituo afya Peramiho

**Na James Mwanamyoto,** SONGEA

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, amesema serikali imeahidi kutoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Peramiho.

Ujenzi wa kituo hicho ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyoyatoa baada ya Mbunge wa Peramiho, Jenista Mhagama. kuwasilisha ombi la kujengewa kituo cha afya.

Ndejembi alitoa ahadi hiyo kwa wananchi wa Peramiho kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Angellah Kairuki, baada ya Dk. Mpango kumpatia fursa ya kuzungumza na wananchi hao.

Ndejembi alisema kwa heshima na maelekezo ya Makamu wa Rais, fedha hiyo itatolewa mapema iwezekanavyo ili kuwezesha ujenzi wa kituo cha afya ambacho kitaboresha utoaji wa huduma za afya kwa jamii.

"Ujenzi wa kituo cha afya unatokana na jitihada za serikali pamoja na Mbunge wa Peramiho, Jenista Mhagama, ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi wake," alisema.

Aliongeza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni atapeleka magari mawili ya kubebea wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, ikiwa ni mwendelezo wa maboresho ya utoaji wa huduma za afya katika Hamashauri hiyo.

# Waziri ataka elimu upandishwaji hadhi vijiji

**Na Munir Shemweta, BI-HARAMULO**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka ofisi za ardhi kufuata taratibu na kutoa elimu kwa wananchi hasa katika ardhi za serikali za vijiji zinapopandishwa hadhi kuwa mamlaka za miji.

Waziri Mabula alisema hayo juzi katika eneo la Lusahunga, Biharamulo mkoani Kagera alipokwenda kutatua mgogoro wa ardhi baina ya Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge na serikali ya kijiji cha Lusahunga.

Mgogoro huo umeibuka baada ya serikali ya kijiji cha Lusahunga kutaka sehemu ya eneo lililoombwa na Kanisa Katoliki kwa madai kuwa ndiyo yenye mamlaka.

Hata hivyo, Tangazo la Serikali Na. 76 la mwaka 1996 lilitangaza eneo hilo kuwa mamlaka ya mji na kulifanya kutoka katika sheria namba 5 ya vijiji na kwenda sheria ya mipango miji.

Sheria Na. 8 ya mipango miji ya mwaka 2007 inaipa mamlaka halmamshauri ya wilaya kusimamia mpango wa uendelezaji, kufanya serikali ya kijiji kutokuwa na mamlaka tena ya kugawa ardhi.

"Maeneo ya vijiji yanapopanda hadhi ni lazima taarifa zifike kwa wahusika ili wajue kuwa sasa eneo hili haliko kwetu na liko kwenye mamlaka nyingine," alisema Dk. Mabula.

Alisema wilaya ya Biharamulo ina vijiji vingi vilivyopandishwa hadhi na katika kuepuka migogoro ya aina hiyo, ameelekeza halmashauri ya wilaya kupita kijiji kwa kijiji kuelimisha wananchi kuhusu mabadiliko hayo.

"Ninaelekeza mkawafahamishe kwa maandishi viongozi wa serikali za vijiji vilivyopandishwa hadhi kuwa hawaruhusiwi kugawa ardhi tena na kama watahitaji kwa ajili ya shughuli za Kijiji, basi watawasiliana na ofisi ya mkurugenzi kwa kuwa mamlaka ya usimamizi wa utawala wa ardhi hayako kwao tena bali halmashauri ya wilaya," alisema Dk. Mabula.

Alisema, watumishi wa sekta ya ardhi wakifuata taratibu sambamba na kuwafahamisha wananchi mabadiliko yanayotokea kwa vijiji vinavyopandishwa hadhi, hakutakuwa na migogoro na wakati huo huo, shughuli katika maeneo hayo zitakuwa zimewezeshwa.

"Eneo lako likipimwa na kupata hati unaweza kuitumia kuchukulia mkopo benki kwa kuwa ardhi yako itakuwa imepanda thamani na hata unapotaka kuuza ni tofauti na yule asiye na hati," alisema.

Kuhusu mgogoro kati ya Kanisa Katoliki na Serikali ya kijiji cha Lusahanga, Dk. Mabula alitaka makubaliano yaliyofikiwa baina ya pande hizo mbili ya Kanisa Katoliki kupatiwa ekari 50 yaendelee na kusimamiwa na mkuu wa wilaya. Alisema ekari 95 zilizobaki zitakuwa chini ya halmashauri ya wilaya ya Biharamulo na kama kijiji kitataka eneo, kinapaswa kuomba huko.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania watumie fursa mkutano wakuu wa AU Dar

**TANZANIA** kuanzia Jumanne ijayo, inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika (AU) utakaojadili uwekezaji katika rasilimali watu. Kama wahenga wasemavyo mgenii njoo mwenyeji apone, nidhahiri kwamba mkutano huo utaleta neema kwa Tanzania katika masuala mbalimbali yua kiuchumi na kijamii.

Mkutano huo utakaohudhuriwa pia na mawaziri wa sekta za rasilimali watu ni wa kwanza kufanyika nchini na Afrika kwa ujumla na ajenda yake ni ukuaji wa uchumi imara kwa nchi za Afrika katika kuongeza tija kwa vijana kupitia kuboresha ujifunzaji na kukuza ujuzi.

Wakati maandalizi ya mkutano huo utakaofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) yakiwa katika hatua za mwisho, baadhi ya viongozi akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ambaye ndiye mwenyeji wameanza kupiga debe kwa Watanzania kuchangamkia fursa.

Katika kupigia debe fursa hiyo, Chalamila amewataka Watanzania hususan wajasiriamali na wafanyabiashara kutumia fursa hiyo kukuza vipato vyao kupitia bidhaa na huduma watakazozitoa kwa washiriki. Sambamba na kuchangamkia fursa, amewataka pia wananchi kuutumia mkutano huo kujenga taswira nzuri ya nchi ambayo tayari Rais Samia Suluhu Hassan ameijenga kupitia hamasa kwenye sekta mbalimbali ikiwamo utalii.

Aidha, katika hamasa hiyo, chalamila amesema mkutano huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ni muhimu katika kujenga utalii wa hoteli, fukwe na utalii wa vyakula, hivyo wananchi hususan wakazi wa Dar es Salaam, wanapaswa kutumia fursa hiyo ili kuongeza kipato na kukuza uchumi wa mkoa huu. Pia kwa wenye hoteli, ni nafasi yao kujitangaza kutokana na ukweli kwamba zaidi ya hoteli 40 zitatumiwa na wageni, hivyo hii ni fursa ya utalii wa mikutano.

Licha ya utalii mikutano, ubora wa huduma na hali ya usafi katika hoteli hizo pamoja na ukarimu, vinaweza kuwa vivutio katika kuwafanya wageni kutoka mataifa mbalimbali kufikia watakaopokuja tena kwa shughuli mbalimbali.

Kwa mantiki hiyo, wamiliki na wafanyakazi wanapaswa kuonyesha weledi katika huduma na ukarimu ili kuwafanya wageni kuzitangaza watakaporejea makwao na hatimaye kupata wateja zaidi siku za usoni. Wamiliki hao wanapaswa kutambua kwamba chema chajiuza kibaya chajitembea, hivyo wahakikishe wanatoa huduma zenye viwango vya hali ya juu.


Ni dhahiri kwamba mkutano huo ni fursa nzuri kwa wajasiriamali wa Tanzania kutangaza bidhaa zao kupitia maonyesho ya bidhaa yatakayofanyika katika eneo la mkutano. Jambo la muhimu kwa wajasiriamali hao ni kuhakikisha wanakuwa na bidhaa bora ambazo zinaweza kuwa kichocheo cha kupata masoko katika nchi wanachama wa AU na nje ya mipaka ya Afrika kwa ujumla.

Katika mikutano kadhaa iliyopita iliyofanyika eneo utakapofanyikia mkutano huo, wafanyabiashara mbalimbali walitumia fursa katika kutangaza bidhaa zao na kujinadi ili kupata masoko. Katika baadhi ya mikutano hiyo, walikuwapo wajasiriamali kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika kama vile Ethiopia na Sudan ambao walitumia majukuwaa hayo kuonyesha bidhaa zao zikiwamo za asili.

Kutokana na kuwapo kwa fursa hiyo, wajasiriamali wazawa wanapaswa kufanya mambo kwa viwango vya juu ikiwamo klubadilishana uzoefu na kujenga uradiki na wenzao kutoka nje ili kupanua wigo wa shughuli zao ndani na nje ya nchi. Ni imani kwamba fursa huiyo itatumika kikamilifu na kuinua pato la mtummoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mabinti na wanawake endeleeni kuchangamkia fursa za kiuchumi

**MABINTI** na wanawake ni kundi ambalo limekuwa likikumbana na vikwazo mbalimbali, vikiwamo vya ukatili wa kijinsia hasa upande wa kiuchumi, hali inayosababisha likwame kupiga hatua za kimaendeleo.

Lakini katikati ya kikwazo hicho, juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanyika kwa ajili ya kulikomboa kundi hilo kiuchumi, ikiwamo kulipa mafunzo yakiwamo ya ujasiriamali.

Kwa sasa kundi hilo limeanza kuwa mstari wa mbele kuchangamkia fursa hizo za mafunzo yakiwamo ya ufundi wa kushona nguo, kutengeneza mkaa mbadala na elimu kuhusu ujasiriamali.

Lakini pia linakuja suala la fursa ya mikopo ya fedha kutoka taasisi za kifedha, kundi hilo limo, linachukua hatua hizo, ili kupata fedha za kufanyia biashara ili kujiimarisha kiuchumi.

Kwa mfano, hivi karibuni vijana wa kike 3,650 walikuwa miongoni mwa watu 5,650 waliofaidika na mafunzo ya ufundi na aina mbalimbali ukiwamo wa kushona nguo, kutengeneza mkaa mbadala na ujasiriamali kutoka Kituo cha Sauti ya Jamii Kipinguni, jijini Dar es Salaam.

Pamoja na ujasiriamali, mafunzo hayo yalijikita zaidi katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, kwani ukatili wa kijinsia unagusa pia suala la uchumi.

Mwenyekiti wa kituo hicho Fatma Talib, katika idadi ya watu wote 5,650 waliofaidika na mafunzo hayo, vijana ni 3,650 huku wa kike wakiwa ni 2,500, wa kiume 1,150, huku vijana wa kike wakionekana kuwa wengi zaidi.

Binafsi ninauona wingi huo kama dalili ya kutambua kuwa wao pia wana uwezo wa kufanya kile ambacho wanaume wanakifanya, hasa kuchangia katika shughuli za kiuchumi kwenye familia.

Katika hilo, ninawatia moyo kuwa waendelee kusimama imara kutafuta fursa za kuwawezesha kiuchumi, ili hatimaye waweze kujisimamia na kuachana na kaulimbiu ya kusubiri kuwezeshwa.

> **Pamoja na ujasiriamali, mafunzo hayo yalijikita zaidi katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, kwani ukatili wa kijinsia unagusa pia suala la uchumi.**

Ikumbukwe kumekuwapo na kaulimbiu ya 'mwanamke akiwezeshwa anaweza', badala yake iwe ni kwamba mwanamke anaweza bila kuwezeshwa, hasa kupitia fursa mbalimbali wanazopata za mafunzo ya ujasiriamali na hata kupata mkopo kutoka katika taasisi ya fedha.

Kupitia njia hiyo, hata ukatili wa kijinsia unaweza kupungua ndani ya jamii, kwani upo wa aina nyingi ukiwamo wa kiuchumi ambao mume anaweza kumnyima mkewe fedha za kujikimu au kufanya biashara. Matokeo yake ni kunyanyasika au wengine kwenda kutafuta mikopo ya roho mkononi na mingine ya aina hiyo ambayo sasa inapigiwa kelele kutokana na riba kubwa inayoumiza wakopaji.

Kitendo chao cha kufikia hatua ya kwenda kukopa fedha hata kwenye riba kubwa, kinaonyesha kuwa wana nia ya kujikwamua kiuchumi, hivyo jambo la muhimu ni kuendelea kuwapa fursa za mafunzo ya ujasiriamali.

Ujasiriamali kwa sasa ndio wenye nafasi kubwa kuanzia kwa mama lishe na biashara nyingine ambayo wamekuwa wakiifanya, kwa ajili ya kujiongezea kipato ili kuondokana na ukatili wa kijinsia.

Hata Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ilishawashukia wanaotoa mikopo inayoumiza wanawake na wakati mwingine kusababisha migogoro katika ndoa.

Pamoja na hayo, jambo la msingi ni hilo la kuchangamkia fursa za mafunzo yakiwamo ya ujasiriamali ili kupata maarifa na ujuzi wa kuweza kufanya shughuli za kiuchumi bila usumbufu.

Kwa kuwa kuna vikundi ambavyo vimeonyesha nia ya kuwashika mkono wanawake na mabinti, ninadhani ni wajibu wao kushikamana ili waweze kunufaika kupitia fursa za mafunzo ya ujasiriamali wanayopata.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Nini chanzo mikataba mibovu tunayoumizwa?



Pascal Mayalla

KUNA msemo wa Kiswahili usemao "Mwendapole, hajikwai, akijikwaa, haanguki, na akianguka, haumii." Tanzania ni nchi ambayo tuko kwenye mchachakamchaka wa kuijenga nchi yetu na kuiletea maendeleo. Mchakamchaka ni mbio za mwendo wa pole, hivyo kanuni ya mwendapole hajikwai, ilipaswa kutumiwa, lakini katika mchakamchaka wetu, kwa nini Tanzania tunajikwaa, tuna anguka na tunaumia?

Kwa maoni yangu, sababu pekee inayotufanya tujikwae, tuanguke na tuumie ni kwamba hatuangalii pale tulipojikwaa. Tukijikwaa, tukaanguka, tukiumia ni kuamka na kuendelea na mchakamchaka wetu, huku tukigugumia na maumivu yetu bila kuangalia tulijikwaa wapi.

Unapojikwaa, ukaanguka, ukaumia, usiamke tu na kuendelea na mbio zako bali amka, fanya tathmini kidogo kwa kurudi nyuma kuangalia umejikwaa wapi, ndipo uendelee na safari yako usije ukajikwaa tena pale pale, ukaanguka na ukaumia.

Unapopatwa na tatizo lolote, hatua ya kwanza ni kujitambua kuwa una tatizo. kujikubali kuwa jambo fulani ni tatizo, kitendo cha kutambua tu kuwa kuna tatizo mahali, ni hatua ya kwanza ya kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

Mimi ni mwandishi wa habari wa kujitegemea kwa kujitolea. Baada ya kuhudumu kwenye tasnia ya habari kwa miaka 10, nilikwenda kusomea sheria na baada ya kuhitimu, niliendelea kuhudumu katika tasnia hii. Kwa sasa nimehudumu katika tasnia ya habari kwa takriban miaka 30 nikiwa mwanahabari na mwanasheria na nikiwa wakili wa kujitegemea.

Tangu nimekuwa wakili, jicho langu limebaini tatizo kubwa linalotukabili nchi yetu, linalosababisha tunajikwaa, tunaanguka, tunaumia, si siasa, si katiba, si sheria, taratibu na kanuni bali ni sisi wanasheria.

Hata hizi kelele zote za wanasheria nguli, wabobezi na wabobevu kuhusu hii IGA ya DPW na bandari zetu ni uthibitisho wa tatizo hili, hivyo hoja zote zinazoibuliwa kuhusu mkataba huu si za kuzipuuzia.

Katiba yetu ya sasa ina matatizo yaliyosababishwa na wanasheria na si wanasiasa. Baadhi ya sheria zetu zina matatizo yaliyosababishwa na wanasheria wetu. Baadhi ya mikataba ya kimataifa tunayoingia ina matatizo na mwisho wa siku tunajikuta kama taifa, tunajikwaa, tunaanguka na tunaumia kutokana na udhaifu wa wanasheria wetu.

Tanzania tunaumizwa, tunafunguliwa mashtaka kwenye vyombo vya usuluhishi, tunashindwa na tunatozwa tozo za mabilioni ya fedha kwa dola za Marekani. Kila tunaposhindwa kesi na kutozwa tozo, huwa tunagoma kulipa na kusema wazi kuwa hatulipi.

Kwenye hili, namwomba sana Rais wetu Samia Suluhu Hassan, Watanzania tuelezwe ukweli hata uwe mchungu vipi kuwa japokuwa tunavimba na kujimwambafai kuwa hatulipi mwisho wa siku huwa tunalipa kimyakimya na Watanzania hatuambiwi.

Nashauri tuambiwe tuu. .Ndege zetu zinapozuiwa kukazia madeni haya, tunapozikomboa, tuwe tunaelezwa ukweli zimekombolewaje?

Kwa maoni yangu, haya yote ni matokeo ya kazi ya wanasheria wetu. Tanzania tumeianza wiki hii kwa Habari mbaya kutoka Marekani kwamba tumeshindwa kesi, tunadaiwa dola za Marekani zaidi ya milioni 100 ambazo ni sawa na zaidi ya Sh. bilioni 250 za Kitanzania. Sijui na hizi tutasema hatulipi lakini mwisho wa siku ni lazima tulipe.

Tuzo hii imenitafakarisha sana kama Tanzania tulipitisha sheria kuwa kwenye uwekezaji hakuna mashauri yoyote kusikilizwa nje ya nchi! Sheria yetu inasema mashauri yote yatasikilizwa hapa hapa nchini na kwa kutumia sheria za Tanzania. Sasa haya mashauri yanaendelea vipi kupelekwa nje?

Hii maana yake ama tuna sheria mbovu ambazo hazitekelezeki au tuna wanasheria wabovu wanaotunga sheria mbovu, zinazotupa mikataba mibovu na mwisho wa siku tunaishia kushindwa na kutozwa tozo hizi za ajabu ajabu.

Upande mwingine wa sarafu ni ama tuna sheria mbovu za mikataba mibovu au kama sheria ni nzuri, basi tuna wanasheria wabovu wasio na uwezo wa kushauri mambo mazuri ya kufanya.

Kwahiyo serikali yetu inavunja mikataba kinyume cha sheria na mwisho wa siku tunashitakiwa na tunaishia kuumizwa kwa kushindwa kesi kutozwa tuzo ambazo lazima tulipe kwa kupenda au kulipishwa kwa lazima pale ndege zetu zinapozuiwa.

Kabla ya kuvunja mkataba wowote, serikali yetu inaomba ushauri wa kisheria kufanya kitu kinachoitwa 'mitigation'. Wanasheria hawa huishauri vibaya serikali yetu na mwisho wa siku, tunaishia kuumizwa.

Naomba niwaonyeshe mifano miwili Tanzania tulivyoumizwa na baadhi ya hizi tuzo ili kuwafungua macho Watanzania kuwa tuzo hizi si chanzo, ni matokeo bali chanzo ni mikataba mibovu, hivyo kutoa uhalali kwa nini Watanzania wanataka mkataba wa bandari yetu uwe mzuri.

Masuala ya Richmond, Dowans, tukaunda tume, ikatoa matokeo kwa mbwembe kuwa Richmond ni kampuni hewa hata tukivunja mkataba, hatutashtakiwa popote.

Tukamfanya Edward Lowassa awe mbuzi wa kafara, tukavunja mkataba. Tukashtakiwa tukashindwa, tukatozwa tozo. Waliotushauri tuvunje mkataba wakajiapiza 'over my dead body' hatulipi. Tulilipa kisiri siri kila senti. Hawa wanasheria walifanywa nini?

Mitambo ya Richmond ikanunuliwa na Simbion, tukaingia nao mkataba ule ule na tukawalipa. Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli alipoingia tukavunja mkataba, tukashitakiwa, tukashindwa, tukatozwa tuzo, JPM akagoma hatulipi. Mama kaingia, tumelipa fasta fasta, kimya kimya. Wanasheria waliotufikisha hapa walifanywa nini?

Tanzania tutaendelea kufanywa shamba la bibi na kichwa cha mwendawazimu na mikataba hii na wanasheria hawa hadi lini?.

**Mungu ibariki Tanzania**
**Paskali**
**0754270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kwa hapa Tume ya Hakijinai imecheza vyema



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MIONGONI mwa mambo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameyafanya katika kuthibitisha dhana ya uongozi bora ni kuunda Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuimarisha Taasisi za Hakijinai.

Tume hiyo chini ya Jaji Mkuu mstaafu, Othman Chande, imefanya kazi kubwa ya kuangalia ni jinsi gani hakijinai imekuwa ikitendeka nchini, hasa baada ya kupita na kuzungumza na wananchi ambao ndio walengwa.

Kati ya mambo makubwa yaliyogunduliwa na tume ni lile la kamatakamata ya Jeshi la Polisi lakini pia la madaraka ya wakuu wa wilaya na wa mikoa, hasa wawapo katika majukumu yao ya utendaji kazi.

Haya ni masuala yanayogusa watu moja kwa moja katika maisha yao na hakika kama mapendekezo ya tume yatafanyiwa kazi, basi Tanzania itakuwa mahali pazuri pa kila mtu kuishi kwa amani na usalama.

Tumeshuhudia polisi wakikamata watu wenye na wasio na hatia na kwa kipigo na hata kwingine kufikia kuwapa kilema cha maisha na hata kuwapora maisha, kwa sababu ambazo hata hazina mashiko na ni nje ya sheria.

Inajulikana kabisa, ni nini anachopaswa kufanya askari polisi anapoamua kukamata mtuhumiwa, ambacho ni kumgusa begani mtuhumiwa na kumweleza tuhuma zake na kumwomba kuongozana naye kunakohusika kwa hatua zaidi.

Ingawa askari anaruhusiwa kutumia nguvu kidogo endapo kuna dalili za mtuhumiwa kukataa kutii amri bila shuruti, lakini si kiasi cha kumjeruhi au kumwodolea haki yake ya kuishi kama ambavyo ilishapata kutokea mahali.

Kwa wakuu wa wilaya na mikoa, huko nako hali haikuwa nzuri kwani ilifikia wakati kama alivyosema mmoja wa wajumbe wa tume, Balozi Ombeni Sefue, inatokea mkuu wa wilaya kutamani 'demu', anatumia maguvu kumpata hata kama kwa kumweka ndani mpenzi wake.

Wakuu wa wilaya na mikoa, mara nyingi hata kwenye mikutano ya hadhara, walifikia hatua ya kutoa amri ya kukamatwa mtu aliyesigana naye kwa hoja na kujisikia kumwaibisha na kumweka ndani hata zaidi ya saa 48.

Kuna mmoja wa wakuu wa mikoa alipata kuvamia kituo cha televisheni usiku na kutaka kulazimisha kipindi kurushwa kwa maslahi yake na kusababisha taharuki si tu kwa watumishi wa kituo hicho, bali hata kwa wapenda amani wote.

Yuko mkuu wa wilaya aliyeamua kuvamia duka la mfanyabiashara na kumlazimisha kutoa fedha akimtishia hata kumpeleka kituo cha polisi huku akisingizia kupata maagizo kutoka juu, kwa maana kwenye mamlaka ya uteuzi.

Hali kadhalika, alitokea mkuu wa wilaya akavamia shule na kupora madaraka ya walimu na kuchapa wanafunzi kana kwamba walimu wa shule husika walikuwa wameshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Tunakumbuka mkuu wa mkoa alivyoamua kumkaripia mkuu wa wilaya hadharani, ikiwa ni sehemu ya kuonyesha mabavu aliyo nayo kama ambavyo mkuu wa wilaya fulani alivyomfokea hadharani mkurugenzi wa halmashauri yake eti kwa kuchelewa ziara!

Yote haya tume iliyaona kama ni upungufu wa kiutawala na kimaadili na kupendekeza madaraka waliyonayo polisi na viongozi hawa wa wilaya na mikoa, yapunguzwe kama si kuondolewa kwani ni kinyume na dhana ya utawala bora.

Pengine tatizo limejikita katika usimamizi wa Jeshi la Polisi kiasi cha kuonekana ni adui na si walinzi wa usalama wa raia na mali zake, lakini pia uteuzi wa viongozi bila uchunguzi unaoitwa kwa Kiingereza 'vetting'.

Siku za karibuni, uteuzi umekuwa ukifanywa kwa kuangalia nani anajikomba kwa nani au nani ni 'chawa' wa nani bila kutazama uwezo na sifa za kimaadili, matokeo yake mtu anadhani akijikomba kwa kuwa hana sifa wala uwezo, basi ataula.

Tulipata kushuhudia huko nyuma, mtu alishatumbuliwa nafasi kubwa lakini akarejeshwa baada ya kujitokeza kunga mkono hoja ya mamlaka ya uteuzi. Matokeo yake ndiyo hayo ya kujiona ni wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama wakati hicho si cheo chao.

Iendelee kueleweka tu, kuwa hawa ni wenyeviti wa kamati za usalama za wilaya au mikoa, lakini ipo haja pia ya kuwatenganisha polisi na viongozi hawa wa kisiasa, ili polisi wawajibike moja kwa moja kwa wakuu wao wa maeneo.

Hiyo itasaidia pia wakuu wa wilaya na mikoa kuacha kuzunguka kwenye ziara zao na kundi la maaskari kwa maana ya uenyekiti wa kamati za ulinzi na usalama, badala ya kuwaacha waendelee na majukumu yao ya kiulinzi na usalama. Alamsiki!

# Miaka 60 ya JKT na ndoto za Samia kiuchumi

Na Mwandishi Wetu

KILA Julai 10, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) huadhimisha uwapo wake nchini tangu lilipoanzishwa na Rais wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Julai, 1963.

Kwa mwaka huu, JKT imetimiza miaka 60 tangu kuasisiwa kwake. Sherehe za maadhimisho hayo zilifanyika katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma na mgeni rasmi alikuwa Rais Dk Samia Suluhu Hassan.

Mkakati wa kuanzisha jeshi hilo ulianza kufanyiwa kazi Aprili 19, 1963 ikiwa ni maafikiano ya Baraza la Mawaziri la Serikali ya Tanganyika chini ya Mwalimu Nyerere kwa lengo la kutafuta namna ya kujenga mbinu za kujikomboa kiuchumi tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961.

Karata ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, ilikuwa na dhamira madhubuti ya kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanajengewa uwezo katika fursa za kujikomboa wao na taifa kwa ujumla.

Hivi sasa, taifa linashuhudia mazuri haya kutoka JKT kutokana na watoto wa Kitanzania wanaotoka shuleni kujiunga na jeshi hili kabla hawajaendelea na masomo ya elimu ya juu.

JKT ilianzishwa kama chombo kitakachokuwa na dira ya kunoa vijana kufundishwa maadili, upambanaji wa kutafuta fursa sambamba na kupandikizwa uzalendo katika jamii.

Tangu wakati huo, kumekuwa na maboresho kadhaa ya JKT, ikiwamo namna ya kupatikana vijana. Sheria ilibadilishwa kutoka watoto wa darasa la saba hadi kidato cha nne mwaka 1966.

**MABADILIKO MAKUBWA**

Mabadiliko ya JKT hayakuishia hapo kwani mwaka 1975 yalifanyika maboresho kwa kuamua kuliunganisha jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Hatua hiyo ilitoa nafasi ya kuamua JKT iwe ndani ya kamandi zilizo chini ya JWTZ na kuainisha majukumu yake mengine kuwa ni pamoja na kuwafundisha vijana kulitumikia taifa katika nyanja za kijamii, maendeleo ya uchumi na ulinzi wa taifa.

Majukumu mengine ya JKT yakawa kutoa mafunzo ya msingi ya kijeshi kwa vijana ili kuwawezesha kufikia sifa ya kujiunga katika vyombo vya ulinzi na usalama kama vile JWTZ, Polisi, Usalama wa Taifa na Magereza, bila kusahau ushiriki kikamilifu katika medani ya ulinzi wa taifa.

JKT pia imekuwa katika ari nzuri ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya kiuchumi kama vile kulinda madini ya Tanzanite, Mererani, kujenga Mji wa Serikali Mtumba na ujenzi wa Ikulu ya Chamwino iliyozinduliwa mwaka huu.




Meja Jenerali Rajabu Mabele

**NDOTO ZA SAMIA**

Akizungumza katika maadhimisho ya Miaka 60 ya JKT, Rais Samia alisema mkakati uliopo kwa sasa ni kuijenga JKT iliyokuwa ndoto ya Hayati Nyerere kuhakikisha kila kijana anayemaliza kidato cha sita kuingia JKT kabla hajarudi kuendelea na maisha ya elimu ya juu.

"Tunataka idadi ya wanaochukuliwa kujiunga na JKT iongezeke kila mwaka kulitumikia jeshi kwa hiari kwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa maslahi ya Watanzania wote.

"Tangu miaka ya 1960, jeshi hili limekuwa likitekeleza mpango thabiti wa kuwajengea vijana wetu msingi wa kujitambua, kulitambua Taifa pamoja na utayari wao kuijenga nchi yetu," alisema.

Rais Samia aliikumbusha jamii na JKT kuhusu dira ya matumizi ya vijana ili wawe tofauti kati ya waliopitia JKT na ambao hawajafanikiwa kujiunga na jeshi hilo hasa kwenye suala la nidhamu, kujituma na uadilifu katika jamii. Mkakati mwingine ambao Rais Samia anaikumbusha JKT kuusimamia ni suala la uzalendo kwa vijana ili uongeze ari na utayari wa kulitetea taifa hasa katika kipindi hiki cha kuongezeka vitendo visivyokuwa vya kizalendo ndani ya jamii.

"Tunataka vijana walibebe taifa ndani ya moyo wao na si mdomoni kwa dhamira ile ile inayokusudiwa kuona nchi yetu inaenda vizuri. JKT imechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa kwa kuwaleta pamoja vijana wenye dini, makabila na itikadi tofauti," alisema.

Rais Samia anasema JKT inafanya vijana wawe pamoja na kushirikiana katika makundi yao ujenzi wa uchumi kutokana na kupata mafunzo na ujuzi mbalimbali. Ujuzi huo kwa vijana ni jambo nyeti hasa kwa wale wanaodhani usomi na taaluma zao zinawaweka mbali na kazi za mikono kama ilivyo dira ya serikali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa JKT kuelekea dira ya Taifa ya mwaka 2025 inayotoa picha ya kujenga uzalendo, utaifa na kuimarisha umoja.

Mpango wa Tatu Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano utakaotekelezwa nchini ambao unatarajiwa kumalizika mwaka 2026/27, kimsingi unatoa wajibu na taswira ya kutumia rasilimali za ndani ili kujitosheleza na kuondoa utegemezi.

Miongoni mwa mambo yanayopewa kipaumbele ni pamoja na kuimarisha vyuo vya ufundi na ufundi stadi likisimamiwa kikamilifu na JKT, chini ya Amri Jeshi wake Mkuu, Rais Samia.

Aidha kasi na mwitikio wa vijana kujiunga na jeshi hilo unatoa dira nzuri kwa kizazi cha sasa kinachokwenda kuvuna mambo mengi ya kwenda kuyatumia pindi watakapoingia kwenye soko la ajira.

Zaidi ya vijana 52,000 walijaza fomu za kujiunga na JKT, tofauti na mwaka jana ambao walikuwa 30,000 tu, huku jambo la kujivunia ni kuwa idadi hiyo ilibebwa yote.

Rais Samia anasema serikali itafanya kila jitihada kuiwezesha JKT ili vijana wengi zaidi wapitie kwenye jeshi hilo kwa kupitia program zake zenye malengo madhubuti ya kujenga kesho ya vijana wa Kitanzania (BBT).

Vijana watatelekezwa kwenye kilimo cha mazao, ufugaji, uvuji na mchakato wa usisimuaji wa Uchumi wa Bluu kwa mustakabali wa Taifa kwa kuanza na ukarabati wa kambi kwa kuunganisha mpango huo wa BBT ili kupokea vijana wale wanaokosa la kufanya pindi wamalizapo chuo na kujikuta wakiishia mtaani bila kuwa na kitu cha kufanya.

Naye Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, anasema jeshi hilo limekuwa chombo muhimu kwa vijana cha kukuza uzalendo nchini.

"Miradi mingi imekuwa ikianzishwa na kuendeleza na JKT bila kusahau miradi ya uzalishaji mali ikiwapo kilimo katika mashamba ya kumwagilia na kutokea kuwa na mchango mkubwa. Kupitia shirika la Suma JKT limekuwa likichangia kwa kiasi kikubwa katika uchangiaji wa pato la taifa bila kusahau kutoa ajira kwa vijana wa Kitanzania,"alisema


Kwa mujibu wa Jenerali Mabele, mafanikio makubwa ya JKT yanawezeshwa kwa kiasi kikubwa na Rais Samia ambaye amekuwa karibu nalo.

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, anasema mafunzo mbalimbali ya vijana kupitia JKT yana lengo la kuwajenga katika mwendo mzuri wa uzalishaji mali nchini Tanzania.

Anasema kufikisha miaka 60 ya JKT kulitokana na mpango wa juhudi wa maendeleo endelevu, sambamba na ulinzi wa Taifa, huku mafanikio hayo yote yakisimamiwa na serikali.



MAISHA
JULAI 23, 2023
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




## KATUNIKA

Ukurasa 16



Ukurasa 14

## MAKANDE YA NYAMA

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15


Wajua zulia huongeza mvuto kwenye nyumba?



# KOMESHA MBA

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | ■ | K | I | N | D | A |
| A | ■ | ■ | ■ | J | ■ | S |
| F | ■ | T | I | I | ■ | H |
| U | F | A | ■ | W | A | O |
| T | ■ | M | I | A | ■ | N |
| W | ■ | B | ■ | ■ | ■ | W |
| A | S | A | L | I | ■ | E |


## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MOI, FAO, OVU, SIE, AMANA, JEMBE, FUMBA, MKOSI, ONGOZWA, ENDELEA

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

TAFUTA NJIA



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Mara aliwaona mtu akimnyoa nywele mwenzake wakiwa chini ya mti. Alipoona watu hao John alianza kulia huku akizishika nywele zake.

Mama: John unalia nini mwanangu, mbona tulikuwa tunatembea vizuri?

John: Mama si umewaona yule mtu akimnyoa nywele mwenzake naogopa sana

Mama: Kwa nini?

John: Mwalimu alisema ukiona mwenzako ananyolewa, wewe tia maji kichwani

Mama: We John huo ni msemo tu, unamaanisha kile kinachompata mwenzako kinaweza kukupata na wewe, hivyo usimcheke.

John: Kumbe

**SWALI**

Zao la Kakao linalimwa wapi nchini Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mambo mke anapaswa kuyafanya

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa katika familia zetu ili maisha yaendelee. Mfululizo tumejadili kuhusu wakwe, mashemeji na mawifi, na jinsi ya kuchukuliana na mke ndani ya familia.

Leo nikazie kwa kuangazia mambo anayopaswa kufanya mke. Wanawake walioolewa wanapaswa kuchukua muda mrefu kusoma na kuelewa kipengele hicho.

Mke anapaswa kumshukuru Mungu kwamba mumewe yupo hai na ni muhimu ajiandae kwa ajili ya siku za usoni. Kwa kuwa mumeo sasa yupo, anza kujiandaa jinsi ya kuhudumia nyumba au familia pale atakapokuwa ameondoka.

Si kana kwamba tunaombea kifo, bali hekima ya kujiandaa ni ya muhimu kwa mwanamke. Ukitafakari mambo yafuatayo, utajihesabu miongoni mwa wanawake walio bora duniani.

Kwanza, kamwe usikubali kuwa mama wa nyumbani maisha yako yote. Mungu amekupa nguvu, utashi, maarifa hivyo shughulisha mikono yako. Neno la Mungu linasema: "Lolote mkono wako utakalopata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe." (Mhubiri 9: 10).

Pia tambua kwamba familia ya mumeo inayojifanya inakupenda sana, sasa inaweza kubadilisha tabia pale watakapogundua kuwa mumeo hayupo tena.

Ni muhimu sasa mama ukajishughulisha ili uwe na mwendelezo wa maisha pale unapojikuta peke yako na watoto wako. Hivi leo, wajane wanaoteseka sana ni wale ambao walikuwa ni mama wa nyumbani kuliko wale waliokuwa na kazi za kufanya.

Kingine, hakikisha kuwa wewe ni mrithi wa mali za mumeo. Hivyo fanya bidii na hekima kuhakikisha kuwa anaandikisha urithi wake kwa jina lako. Kama hutafanya hivyo unaweza kushangaa unanyang'anywa kila kitu na watu wengine pale anapofariki.

Hivyo, mtie moyo na umshauri mumeo aandike urithi wake, lakini fanya hayo yote kwa maombi na hekima. Pia unapaswa kuipenda familia ya mumeo kwani utawahitaji kesho.

Vile vile unapaswa kumpenda na kumtii mumeo kwani ukimchukia, ndugu zake watafahamu siri zake pasipo wewe kufahamu chochote.

Ni muhimu pia kumuombea mume wako aishi maisha marefu. Wapo baadhi ya wanawake wanaofiwa na waume zao wakiwa bado wadogo. Kundi hili hupata mateso makubwa kuliko wale wanaofiwa na waume wakiwa wamezeeka, ambao wana watoto wa kuwatetea!

Kingine muombe Mungu akupe kibali mbele ya macho ya mumeo na kwa familia yake(ndugu zake). Usije ukaenda nyumbani kwao kumsemea kama amekosea.

Kama ukienda utakuwa umejiweka chini ya miguu yao ili wakukandamize. Kama una shida imetokea, nenda kwa mchungaji wenu au washauri wa ndoa wawasaidie.

Omba pamoja na mumeo na usiache mlango wa dhambi kuingia ndani ya ndoa yenu, kwani mshahara wa dhambi ni mauti. Pia jali na kuhudumia familia ya mumeo.

Katika eneo hili la kujali familia ya mume, wanawake wengi wamedhurika kutokana na uelewa finyu, wivu na ukosefu wa hekima ya namna ya kuchukuliana nao ili isiwepo migogoro au migongano isiyokuwa na tija.

Wiki iliyopita nilijadili kwa undani kuhusu mashemeji na mawifi na yale anayopasa kuzingatia mke aweze kuishi nao kwa amani. Wanafamilia hawa ukiwafanyia ubabe, utatahayarika mwenyewe ubaki unashangaa.

Pia kuhusu wakwe nikasema mwanamke hapaswi kushindana nao. Mume ni mtoto wao na wana haki ya kuwasiliana nao kujuliana hali na kwa mahitaji mbalimbali. Pengine chakula au kuuguliwa(magonjwa).

Pia nikatoa mifano ya wadada wawili waliokuwa wakiwadharau mama mkwe na mawifi na nini kiliwatokea. Mmoja alipoteza hata maisha huku mwingine akibakia na maswali mengi kichwani.

Kisa, mama mkwe anamuomba mkamwana hela kidogo amtumie huko Kijijini lakini binti japokuwa anazo, anamnyima. Anasahau mama wa mumewe ni mama yake anapaswa kumsikiliza.

Au wifi amemtembelea lakini hamjali, anamnunia eti amekuja kufuata nini. Ebo! Si amekuja kuwasalimia na wewe ni mke wa kaka? Akiwajulia hali kuna ubaya gani? Kumbuka ugeni wa aina hii huwa unakuja kudadisi, je, unawapenda hata wao au ni kaka yao tu?

Wakigundua huwapendi, ndipo vita huanza. Hata kama hawataka kukufanyia ubaya, ndipo sarakasi linapoanzia. Tuwe makini sana familia mbili zinapoungana kupitia ndoa. ***Tuendelee wiki ijayo: Apasayo kufahamu mume awapo hai. Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Tumepoteza sababu ya kuishi?

MOJA ya mambo yanayoumiza vichwa vya watu wenye uwezo mzuri wa kufikiri na kuhoji mambo hivi sasa ni hili sakata la udanganyifu wa vidonge vya kufubaza makali ya virusi vya Ukimwi, maarufu kama ARV.

Siku kadhaa zilizopita, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, alifichua siri kuhusu hujuma za udanganyifu zinazofanywa na baadhi ya watu kwa kuweka unga wa muhogo katika dawa bandia (feki) za kufubaza makali ya virusi vya ukimwi.

Alisema wako wanaozalisha dawa hizo hivi sasa kwa kutumia hila hiyo, jambo ambalo lina athari kubwa kiafya kwa mtumiaji wa dawa hizo.

Kikwete alifunguka na kulaani udanganyifu huo, alipoalikwa kushiriki hafla ya kuwaaga wapanda mlima na waendesha baiskeli 61, waliokuwa wamejitokeza kuchangia kampeni ya kitaifa ya mapambano ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi kwa kupanda Mlima Kilimanjaro.

Kwangu mimi, hilo ni jambo baya na linalopaswa si tu kukemewa, kusakwa kwa udi na uvumba wanaotengeneza ARV zilizochanganywa unga wa muhogo.

Hakuna tofauti na kuua kwa kukusudia, kunyonga au kujaribu kutoa uhai wa mtu mwingine kwa sababu ya pesa au kiburi cha pesa.

Iko hivi! katika maisha, poteza vyote ila usipoteze matumaini. Ukipoteza matumaini, umepoteza sababu ya kuishi. Kwamba, hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu. Ndiyo!

Rais Mstaafu Kikwete alinukuliwa akisema: "Dawa ni bure, ukisikia mtu anakwambia zinauzwa anakudanganya, hivyo chukueni kwenye vituo rasmi, siku hizi watu wanafanya udanganyifu; wapo ambao wanaweka unga wa muhogo. ...jambo ambalo lina athari kwa afya na haziwezi kumsaidia mhusika. Upo udanganyifu mwingi unaofanyika katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Ni wajibu wa watumiaji kuchukua dawa maeneo yanayoelekezwa na wataalamu wa afya hapa nchini."

Kuhusu vita dhidi ya Ukimwi, Kikwete alinukukiwa akisema serikali imejipanga kuhakikisha inanunua mashine nyingi za kupimia kiwango cha virusi vya ukimwi katika mwili wa binadamu.

Zaidi akasema, mashine hizo zinalenga kusaidia upatikanaji wa dawa kwa wakati na kuendelea kurefusha maisha.

Vilevile Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML),Terry Strong, alinukuliwa akisema kuna haja kwa kwa serikali ya Tanzania, kuongeza jitihada za kutunza nguvu kazi iliyopo kwa sasa.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ummy Nderianga, amejitosa kuwa kiongozi wa pili kukemea udanganyifu huo, akitaka Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) kuonyesha Watanzania namna ambavyo nchi yao inapinga unyanyapaa na ina lengo la kufikia sifuri tatu ifikapo mwaka 2030.

"Tunawapongeza mashuja wote, mafanikio yenu yanadhihirisha kuwa mwitikio wa mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi unakwenda vizuri. Iwapo kutakuwa na dhamira ya dhati kwa kila mmoja wetu na ushirikiano wa pamoja wa kufikia malengo ya kitaifa ya kufikia sifuri tatu, tutakuwa tumefanikiwa zaidi."

Pia, Naibu Waziri huyo, alisema serikali imeweka lengo ambalo kila Wizara na taasisi ya umma inatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya masuala ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi. Alisema katika mwaka 2022/23, TACAIDS ilitengewa Sh. bilioni 14.98 kwa ajili ya masuala ya hayo na mwaka 2023/24 imetengwa Sh. bilioni 25.86.

Kadhalika, alisema serikali ilianzisha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi (AIDS Trust Fund -ATF), kwa lengo la kupunguza utegemenzi wa rasilimali za kufadhili afua za VVU/UKIMWI kutoka nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Ummy, mfuko huo una lengo la kuongeza uendelevu wa huduma muhimu za Ukimwi.

Alisema, pamoja na wadau wengine wa maendeleo ikiwemo GGM, zimewezesha serikali kutoa bure dawa za kufubaza VVU (ARV) kwa WAVIU na kuendelea kuyafikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya kuwa na sifuri tatu, yaani kutokuwa na maambukizi mapya, kutokuwepo kwa vifo vitokanavyo na Ukimwi na kutokomeza kabisa unyanyapaa ifikapo mwaka 2030.

Alisema Machi, 2021 Sh. mil 543.62 ziligawiwa kwa mashirika 20 yanayojishughulisha na utekelezaji wa afua za Ukwimwi nchini, kupitia Halmashauri 20 zilizo kwenye mikoa 10.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela, alisema kurudi kwa vijana hao ni kuonyesha namna gani walifuata maelekezo, taratibu na kanuni za viongozi wao.

Kwa upande wake, Strong, alisema kurudi kwa timu hiyo ni kuonyesha ushujaa wa namna ambavyo Tanzania imejipanga kukabiliana na tatizo hilo.

**•Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI



Juni 6, mwaka huu ilikuwa siku ya furaha kwa Mgusi Wajele na Zainabu Ramadhan, baada ya kufunga ndoa katika Kanisa na Wasabato Kihonda mkoani Morogoro. Ndugu, jamaa na marafiki wanawaombea maisha marefu katika ndoa yao







# MITINDO









# HIVI UNAPENDEZA

WAKATI kipindi cha kipupwe kinakwenda ukingoni, mavazi yanayoendana na hali hiyo haupaswi kuyaepuka kwani kuna baadhi unaweza kuyatumia.

Moja ya vazi linalofaa kuvaliwa hata katika nyakati za hali ya hewa ya wastani ni jaketi iliyotengenezwa na ya ngozi laini.

Jaketi ya ngozi laini ni nzuri kuuweka mwili sawa katika shughuli zako za kawaida kama safari, matembezi ya jioni au kupunga upepo ufukweni.

Kimsingi ndani ya nyumba ni muhimu kuwa na jaketi hasa la ngozi laini, kwani licha ya mwonekano wa kupendeza pia inakujengea kujiamini kutokana na ubora wake.

Wabunifu wamekuwa wakifanya maboresho ya mitindo kila wakati ili kumpatia furaha mtu atakayevaa.

Sifa kubwa ya nguo hizi ni kuwa na uwezo wa kutengeneza joto wakati wa baridi na pia lina mwonekano wa kuvutia pale mtu anapovaa.


Aina hii ya majaketi hayachagui nguo zingine za kuvaa, inapendeza kuvaa na suruali ya jeans, suruali ya kitambaa au nguo ya mazoezi.

Usisahau miguuni ukapigilia viatu vyako vya kutumbukiza kama snika, raba, buti na viatu vingine unavyopenda.

UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# KOMESHA MBA



HAKUNA kitu kinachotia aibu na wakati mwingine kukudhalilisha kama kuwa na utando uliokauka kwenye nywele unaojulikana kama mba.

Kimsingi tatizo hili halitokani na uchafu kama inavyoonekana na wengi, bali husababishwa na ukavu wa ngozi au maambukizi ya fangasi.

Kuondoa tatizo hili, unaweza kutumia shampoo za kuondoa mba, lakini zina kemikali ambayo zitakuletea matatizo ya ngozi. Ni afadhali ukatumia njia za asili.

Maji ya limao

Limao ni njia moja wapo rahisi ya kuondoa mba bila kupatwa na madhara.

Citric acid iliyopo katika limao inasaidia kushambulia visababishi vya fangasi na ina saidia kupandisha ngozi zilizo kufa juu na kukuwezesha kuzisafisha kwa urahisi.

Njia nzuri ya kutumia Limao kuondoa mba ni kwa kufuata njia hizi mbili, kwanza kamua kijiko kimoja cha limao bila kutia chochote, halafu sugua taratibu ngozi yako ya kichwa kwa kutumia maji hayo na uache kwa dakika tano.

Baada ya hapi osha nywele zako kwa kutumia maji ambayo umechanganya na kijiko kimoja cha limao. Fanya hivi kila unapo taka kuosha nywele.

Kitunguu swaumu

Namna nyingine ya kuondoa mba ni kwa kutumia kitunguu swaumu, unaweza kuwaza kuhusu harufu lakini hii ni njia nzuri sana.

Kitunguu swaumu kina antifungal properties ambazo zina nguvu kubwa za kuondoa/kusafisha mba kwa haraka.

Twanga kitunguu swaumu chako na changanya na kikombe kimoja cha maji. Sugulia kwenye ngozi ya kichwa iache kwa muda wa dakika kumi kisha osha na shampoo.



MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Umekula makande ya nyama?

MAKANDE ya nyama ni moja kati chakula kitamu ambacho kinaliwa nyakati zote iwe mchana au usiku.

Hata hivyo chakula hiki si wengi wanakifahamu kutokana na kutojua namna ya kukipika. Leo tutakupa njia namna ya kupika makande ya nyama.

**Maandalizi**

Hatua ya kwanza kabisa kwenye upishi huu ni kuchambua mahindi, maharage au njugu kwa wale wasiotumia maharage na kuyaosha vizuri.

Baada ya kuosha washa jiko na uanze kwa kubandika makande na baada ya dakika 30 uongeza maharage au njugu mawe.

Wakati unasubiri mahindi yaive katakata nyama, osha na uongeza kitunguu swaumu, tangawizi na chumvi kisha uchemshe pembeni mpaka iive.

**Namna ya kuunga**

Makande na nyama vikiiva hatua inayofuata ni kuyaunga kwa pamoja na kutengeneza makande ya nyama.

Hapa utaanza kwa kumenya nyanya, vitunguu, karoti na hoho pamoja na kuandaa tui la nazi tutakalolitumia kwenye chakula chetu.

Kwenye sufuria safi weka mafuta kiasi kaanga kitunguu mpaka kiive, kisha ongeza nyanya na ufunike ziive vizuri.

Baada ya nyanya kuiva ongeza nyama koroga na ufunike kwa dakika tano ichanganyike na nyanya.

Dakika tano zikiisha funua, koroga tena na uongeze makande, chumvi, karoti, hoho na tui jepesi na uache ichemke kwa dakika tano au zaidi.

Pishi lako likichemka ongeza tui la pili zito. Acha ichemke kwa dakika 5 au zaidi kutegemea na wingi wa tui uliloongeza.

Baada ya kujiridhisha na kiwango cha mchuzi unachotaka msosi wako utakuwa tayari kwa kula.

Unasubiri nini? waite marafiki na ndugu wafurahie msosi huu wenye faida nyingi mwilini ikiwamo kukupa nguvu na muonekano mzuri.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Wajua zulia huongeza mvuto kwenye nyumba?

ZULIA ndani ya nyumba ni muhimu sana katika kuchangia mvuto. Japokuwa si la lazima sana, linapowekwa huongeza thamani ya nyumba.

Kuna aina mbalimbali za zulia, lipo kubwa la kutandika sebule yote, la kutumika kutandika sehemu ya kuweka samani pekee, dogo kiasi la kutumia katikati ya meza na dogo kabisa la kutumika mlangoni, korido au bafuni kwa ajili ya kufutia miguu.

Leo nazungumzia zulia linalotandikwa kuendana na mpangilio wa samani za ndani. Mara nyingi tunapolitandika kwenye nyumba zetu, huwa tunakosea vitu vidogo lakini leo tunataka tuangalie namna bora tunapoamua kulitandika.

Ni vyema kabla ya kulitandika, ukahakikisha umelipima kulingana na ukubwa wa eneo zinapopangwa samani ili usiende tofauti na lengo na kuhakikisha miguu ya samani inakuwa ndani ya zulia.

Jambo lingine ni kuhakikisha unachagua linaloendana na miongoni mwa rangi za mapambo mengine ya sebule yako. Kwa mfano, endapo chumba kina muundo wa duara, ni vyema pia zulia litakalotumika kutandikwa liwe na umbo la namna hiyo.



Ni vizuri kuepuka kuweka zulia tofauti na hilo kwa sababu linaweza lisienee au likakosa utulivu au ukalilazimisha kutokana na kutolipima kabla, hivyo likaonekana kama limetuna ovyo.

Kwa chumba chenye pembe nne, nacho kitahitaji kuwa na zulia la muundo huo. Endapo chumba ni kirefu zaidi na chembamba, nunua zulia la kukata kwa kuzingatia mpangilio mzuri wenye vipimo kulingana na namna unavyopanga kuweka eneo lako.

Endapo umeweka zulia la kuenea sebule yote na ni la rangi moja, ni vizuri ukatupia zulia ndogo kwa juu ili kuleta mvuto zaidi. Epuka kufananisha rangi ya zulia na kila kitu kilichoko katika chumba chako.

Tambua kwamba ukichanganya rangi mbili au tatu ndani ya chumba hazichoshi sana na unaweza kupata mwanya mkubwa wa kupendezesha na kufanya mabadiliko ya baadhi ya vitu hususani pazia na urembo mwingine.

Kumbuka kuwa hata usipoweka zulia ndani ya nyumba au sebule lako, hakuna kinachoharibika.

# Holda za miti inapamba nyumba

**Na Restuta James**

WIKI iliyopita nilikueleza namna ambavyo teknolojia imeendelea kuleta mageuzi kwenye nyanja mbalimbali ikiwamo ya mapambo ya ndani.

Leo ninakuletea mageuzi kwenye eneo la mapambo ya ndani kipengele cha taa. Kwenye eneo hili kuna mabadiliko ya matumizi ya vitu asilia kama mawe uliyoyaona kwenye makala ya wiki iliyopita.

Mageuzi hayo hayajaishia kwenye mawe pekee kwani hadi nakshi za magome ya miti zimeingia kwenye samani na vifaa vya umeme.

Taa iliyopo pichani ina aina moja ya mapambo ambayo yanatumika kama 'holder' za taa.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani na vifaa vya umeme, Johnson Ngowi, anasema magome na matawi ya miti yanatumika kutengeneza holder hizo.


Anasema: "Ndio mageuzi yanayoendelea kama unavyoona hii ni holda ya miti, yenyewe ni pambo na wakati huo huo inaleta nuru ndani."

Anasema taa hizo zinapendeza zaidi kwenye kibaraza, ukuta wa koridoni na meza ya kujipambia (dressing table).

Anasema taa hizi zinapendeza zikiwekwa kwenye ukuta wa pembeni na sio juu (kwenye dari)..



# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
MTANIIIIIII MIMI TAYARI, ZAMU YAKO 'USITETEMEKE' NJOO KWEUPE NIKUONE VIZURI
JUKWAANI
UTAFIKA?
MUNGU NDO ANAJUA!
UONGO-ZII
ULIYEMPACHIKA KESI KAONEKANA JANA ANAPANDA BASI LA KWENDA 'SUMBAWANGA'
DUH!
KAKA NAONA MIRADI YA MAENDELEO IMEJIBU!
KAMA UNAVYOIONA 'MAZINDIKO' YANASAIDIA
UNAAMBIWA NDUGUYO YUPO NDANI, UNAULIZA UENDE NA SHING' NGAPI...KWELI?
MWEHU HUYO!
SIO MWEHU FIKIRI KWANZA
MSIMLAUMU SANA KUFUNIKA KOMBE... MWAMBIENI KUWA ASIKARIRI ATALIWA KWELI AKIWA BOYA!
HUWEZI JUA HUENDA KUNA BIASHARA KULE SERO ALIKOSWEKWA NDUGUYE!
UMEBAKIA NA SUTI UNARANDA NAYO NYUMBANI NENDA MBAGALA KWA FETI
WE UNADHANI KIINUA MGONGO KINAKATIKAGA KAMA SALIO LA SIMU?
KAMA HATAKI SI UMUACHE!
ANZA WEWE USIYEHIMILI GUBU!
MKE MPYA NOMA HATA WEWE UNA-ZAMU CHOONI!
WEWE HAPA SI UNAJIKUTA UPO BENKI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...BAHATI HAIJI KWA KUVUNJA NAZI...



Mkazi akiangalia sehemu ya nyumba yake iliyoharibiwa na mashambulizi ya mabomu huko Belgorod nchini Ukraine jana. **PICHA: AFP**

# Madaktari wachapwa bakora Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

TIMU ya madaktari imejeruhiwa baada ya msafara wao kushambuliwa na kisha kuchapwa viboko na watu wenye silaha nchini Sudan.

Kulingana na shirika la madaktari wasio na mipaka, Médecins Sans Frontières (MSF), tukio hilo lilitokea katika mji wa Khartoum, wakati timu ya madaktari ilikuwa ikipeleka vifaa katika Hospitali ya Uturuki kusini mwa Khartoum siku ya Alhamisi.

Katika tukio hilo, watu hao waliiba gari moja huku wakiwaacha madkatari hao wakiugulia majeraha yalitokana na bakora hizo.

Tangu vita vilipozuka katikati ya mwezi wa Aprili, hospitali mbili pekee bado zinafanya kazi kusini mwa jiji hilo ambazo zote zinafadhiliwa na MSF.

Mapambano makali ya kugombea madaraka yamefikia miezi mitatu yakihusisha jeshi na Kikosi cha Msaada wa Haraka (RSF).

Kutokana na vita hiyo, watu milioni tatu nchini kote wamekimbia makazi yao na kwenda ukimbizini nje ya nchi, na idadi kubwa bado wamekwama katika mji wa Khartoum, wakihangaika kupata chakula na dawa.

MSF ni mojawapo ya vikundi vichache vya misaada vya kimataifa ambavyo bado vinasaidia hospitali huko Khartoum na mji wake pacha wa Omdurman, kuweka mfumo wa afya ambao umekuwa katika matatizo kwa miongo kadhaa.

Shirika hilo lilionya kwamba matukio hayo yanaweza kukomesha huduma za msaada kwa sababu usalama umezorota na kukithiri matukio kadhaa ya mashambulio ambayo wafanyakazi wake wakilengwa.

**BBC**

# Brazil yaanza kudhibiti silaha holela kwa raia

**BRASILIA,** BRAZIL

RAIS wa Brazil, Luiz Inacio Lula da Silva, ametia saini amri ya kuzuia umiliki na utunzaji holela wa silaha kwa raia. Hatua hiyo ni kutaka kutengua sheria zilizochochea ongezeko la umiliki wa bunduki zilizoungwa mkono na mtangulizi wake Jair Bolsonaro.

Rais Da Silva amechukua hatua hiyo ikiwa kuna msururu wa hatua za kukabiliana na ghasia mjini Brasilia, baada ya kuripotiwa kwa visa kadhaa vya ufyatuaji risasi shuleni. Amri hiyo ya rais itawafanya watu kumiliki silaha mbili pekee kwa matumizi ya ulinzi binafsi.

Chini ya amri hiyo, mtu yeyote anayetaka kupata bunduki atalazimika kuthibitisha kuwa anaihitaji.

Wawindaji na wanaotumia bunduki katika michezo watapunguziwa idadi ya silaha hadi sita, kutoka 30 walizokuwa wakiruhusiwa kumiliki hapo awali.

Wakati wa utawala wa Bolsonaro umiliki wa bunduki kwa matumizi binafsi uliongozeka maradufu baada ya kulegeza masharti ya umiliki wa silaha.

**DW**

# Crimea yashambuliwa kwa mabomu

**MOSCOW,** RUSSIA

GAVANA wa jimbo la Crimea ambaye anaungwa mkono na Russia, amesema ghala la kutunzia mabomu limeshambuliwa na ndege zisizo na rubani jana.

Baada ya shambulio hilo, mamlaka imewalazimisha watu kuondoka eneo hilo ndani ya umbali wa kilometa tano kwa ajili ya usalama.

Shambulio hilo limesababisha kusitishwa kwa usafiri wa barabara katika daraja linaloiunganisha Crimea na Russia.

Hata hivyo baadaye, ukurasa rasmi wa mamlaka ya Crimea ulitangaza kuwa shughuli za usafiri zimeanza tena baada ya kusitishwa kwa muda.

Gavana huyo, Sergei Aksyonov, kupitia ukurasa wake wa Twitter iliandika kuwa kulitokea mlipuko kwenye ghala hilo huko Krasnohvardiiske katikati ya jimbo hilo.

Hata hivyo, hakuna majeruhi wala uharibifu ulioripotiwa kutokana na shambulio hilo.

Video iliyotolewa na shirika la habari la Russia, ilionyesha wingu nene la moshi wa kijivu katika eneo la tukio.

Aksyonov aliinyooshea kidole cha lawama Ukraine kwa kuhusika na shambulio hilo. Lakini Ucraine haijajibu lolotea kuhusu tuhuma hizo,

Russia iliidhibiti Crimea na kuiweka chini ya utawala wake kutoka kwa Ukraine mwaka 2014 kabla ya kuivamia nchi hiyo miaka nane baadaye. Barabara ya kilometa 19 na daraja linalokatisha baharini hadi Russia, ni kiungo muhimu kwa upitishaji wa vifaa vya kijeshi na linatumika pia na watalii wa Russia wanaokwenda Crimea wakati wa majira ya joto.

Russia inaituhumu Ukraine kwa kufanya mashambulizi kwenye daraja hilo.

Maofisa wa Ukraine wamepongeza mashambulizi hayo bila kukiri kuwa nchi yao imehusika au hapana.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema siku ya Ijumaa kuwa daraja hilo ni eneo muhimu wanalolilenga kwa kuwa ni njia inayotumiwa kusambaza vifaa vya kijeshi vya Russia.

Mashambulizi katika rasi hiyo ya Bahari Nyeusi yamekuwa yakishika kasi katika wiki za hivi karibuni, huku Ukraine ikijibu mashambulizi ya kutaka kurejesha jimbo hilo.

Wakati huohuo, Gavana wa Belgorod Vyacheslav Gladkov, alisema Ukraine ilitumia mabomu ya mtawanyiko kushambulia eneo la mpaka la Belgorod.

Alisema, nchi hiyo ilishambulia kijiji cha Zhuravlyovka kwa roketi zilizorusha mabomu hayo katika tukio ambalo hakuna majeruhi wala uharibifu ulioripotiwa.

Hivi karibuni Marekani iliipatia Ukraine mabomu ya mtawanyiko ili ijilinde na mashambulizi, licha ya ukosoaji mkali nchi za Ulaya.

**DW**

# Afrika Kusini yawasilisha ombi kukamatwa Putim

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

SERIKALI ya Afrika Kusini imetuma maombi rasmi kwa mahakama kutoa hati ya kukamatwa kwa Rais wa Russia Vladimir Putin, iwapo atawasili nchini humo.

Chama kikuu cha upinzani nchini Afrika Kusini, Democratic Alliance, kilisema kuwa kuwasilishwa kwa maombi hayo ni kutekeleza makubaliano ya matakwa yake ambayo chama hicho hapo awali kiliwasilisha ombi kulazimisha serikali kutekeleza agizo la kukamatwa kwa Putin.

Hati ya kukamatwa kwa Putin ilililotolewa mwezi Machi na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) huko The Hague kwenda kwa serikali ya Afrika Kusini.

Afrika Kusini inawajibika rasmi kufuata matakwa ya ICC, na Putin alialikwa kwenye mkutano wa BRICS utakaofanyika Agosti mjini Johannesburg.

Hata hivyo, serikali ya Afrika Kusini ilisisitiza kwamba haikuwa na nia ya kumkamata kiongozi huyo. Hata hivyo, serikali ya Afrika Kusini ilishindwa kupata njia yoyote ya kisheria ya kutotekeleza kibali hicho.

Viongozi wa Afrika Kusini walisema kwa uwazi katika siku za hivi karibuni kwamba walimwomba Putin asiende, na siku ya Jumatano ilitangazwa kiongozi huo hatahudhuria mkutano huo.

**BBC**

MAKALA

# VICHAA WENYE AKILI TIMAMU



Na Magabilo Masambu

WAKATI nikiwa mdogo zamani, palikuwa na hadithi nyingi kuwahusu watu kwenye jamii, hasa baadhi ya wanafunzi wa wakati huo.

Nimewahi kusikia mara kadhaa kwamba mtoto wa fulani amechanganyikiwa kwa sababu akili zimezidi. Nikasikia pia kuna baadhi ya wanafunzi ilikuwa inafika kipindi wanakatazwa kusoma sana kwa sababu eti akili zao ni nyingi, hivyo wakitumia muda mrefu kusoma sana watachanganyikiwa.

Nakumbuka kisa kimoja ambacho kilinifanya nianze kuamini maneno haya. Mwaka 1994, babu yangu aliugua ugonjwa wa kubanwa mkojo, yaani alisikia haja ndogo alipokwenda mkojo haukutoka ukawa ugonjwa kwelikweli, akapelekwa hospitalini pale Kibara-Bunda ikiitwa Namibu wajita tunaita "Nyamibhu".

Alipofikishwa pale akahudumiwa ikiwa ni pamoja na kuwekewa chupa kadhaa za maji.

Tukiwa pale hospitalini akaja ndugu yetu mmoja hivi ambaye kwa wakati huo alikuwa anasoma sekondari lakini alisimama masomo kutokana na ugonjwa wa akili kwa madai kwamba alikuwa na akili nyingi sana.

Alipaswa kusimama masomo kisha zikitulia arudi shuleni. Basi alipopata taarifa kuwa babu anaumwa akaja kumwona na alipofika pale akakutana na aliyekuwa zamu kwa ajili ya kumwuguza.

Jamaa alibeba mkoba ndani ya mkoba akatoa dawa za kienyeji, akamwamru aende akazichemshe mara moja amletee anywe na akasimama hapo mpaka zikaletwa na wakamnywesha.

Baada ya kunywa zile dawa alikojoa damu nyingi sana na baada ya siku chache akatolewa hospitalini.

Dalili zote za yule bwana zilionyesha kuwa ni kichaa lakini mazungumzo yake ndiyo yalikuwa yanawashangaza watu kwa sababu alizungumza na kutenda mambo ya kustahajabisha ambayo hayawezi kufanywa na kichaa wa kawaida japo dalili zote zilionyesha ana tatizo la akili.

Nataka kusema nini? Siku hizi ni kawaida sana kuona mtu akitembea huku akicheka mwenyewe barabarani, kwenye daladala, nyumbani, kazini, darasani na mahala pengine. Kabla sijagundua shida ni nini, nilikuwa najiuliza sana kwa nini hawa watu wanachekacheka wenyewe? Lakini mara zote ukiwaona wanacheka wako peke yao hawana mtu pembeni, kitendo kama hicho na cha kujitenga kinaweza kufanywa na mtu mwenye tatizo la akili.

Imekuwa kawaida pia watu wanaosafiri kwenye basi au chombo chochote cha usafiri, walioketi kiti kimoja kutofanya mazungumzo yoyote na wakati mwingine hata salamu hawasalimiani kutoka mwanzo wa safari mpaka mwisho. Wanashuka hawajaongea chochote.

Kwa mila na desturi zetu za kiafrika hasa za Kitanzania kwa tulivyokuwa tumezoea, mazoea yana tabu.

Ukutanapo na mtu cha kwanza mnasalimiana, kama ni mkubwa utamsalimia shikamoo au habari za saizi na wakati mwingine mnafika mbali zaidi kufahamiana, kushirikishana mnashughulika na nini kama kazi za vipato vyenu. Lakini siku hizi utamaduni huo unakwenda unakufa kwa sababu tu kuna jambo linatufanya tuwe hivyo.

Kuna wakati najaribu kufikiria kama ni ushamba lakini wakati mwingine nasema pengine ni kwa sababu mabadiliko ya teknolojia hatujayazoea, ndiyo maana tunajaribu kuyazoea kwa nguvu, hivyo madhara yake ndiyo hayo.

Simu za mkononi hasa hizi za kisasa zimekuwa chanzo cha kuwafanya watu wenye akili timamu kuonekana vichaa, ndiyo maana nasema ni vichaa wenye akili timamu. Tatizo ni kubwa kuliko tunavyodhani.

Simu zenyewe si tatizo bali ni maudhui yanayopatikana mtandaoni. Uhusiano miongoni mwetu umeuawa na badala yake tunahusiana zaidi na simu zetu kuliko watu tunaowaona. Jambo hili laweza kuonekana la kawaida lakini madhala yake kwa ustawi wa jamii kutokana na utamaduni wetu ni makubwa.

Siku hizi unakwenda nyumbani kwa mtu, akishakukaribisha tu tayari anarudi kwenye simu yake. Mgeni unabaki kutazama katuni na watoto, tena kama ndiyo umetokea kijijini hali inakuwa mbaya zaidi.

Unaweza kujuta kwa nini umekwenda kwa watu. Baada ya muda utaanza kuona aliyeshika simu, akichekacheka kama kichaa lakini ni mtu ana akili timamu. kinachomchekesha ni vituko anavyoviona mtandaoni.

Hali ni mabaya zaidi katika taasisi za elimu ya juu kwa maana ya vyuoni. Karibu kila mwanafunzi unayemwona anatembea kashikilia simu mkononi, anachati, anacheka na kuongea mwenyewe. Umekuwa ugonjwa wa kila mwanafunzi.

Akiingia kwenye daladala akishakaa tu, cha kwanza kutoa ni simu utaanza kumwona tu akitabasamu. Wengine wanajisahahu wanacheka kwa sauti lakini abiria mwenzake aliye naye kwenye kiti kimoja hawaongei wala hawakusalimiana.

Nadhani kuna umuhimu wa kupunguza kasi hii ya utumiaji huu wa simu.

Tunakoelekea hatutajuliana hali kabisa, kama ambavyo wenzetu wanaishi huko kwao.

Mwingine anaweza kusema kwani lazima kufahamiana? Ukiona mtu anasema hivyo, tayari mawazo ya Kiafrika na Kitanzania yameshamtoka. Anajiona mzungu angali na ngozi nyeusi.

Utu wetu utaharibika, kuthaminiana kutakufa na mwisho tutaishi kama wanyama.

Tusijaribu kuwa vichaa wakati tunazo akili timamu kwasababu ambazo hazina msingi. Wanaotengeneza hivyo vichekesho, wametumia muda wao vizuri ndiyo maana tunawatazama nasi tutumie muda wetu vizuri ili kutazamwa kama wao.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mazoea yananikondesha, wimbo wa maumivu ya kukimbiwa na mpenziwe*



Na Adam Fungamwango

BENDI ya Msondo Ngoma Music ilifyatua kibao kiitwacho 'Kilio cha Mtu Mzima,' utunzi wake Hayati TX Moshi William mwanzoni mwa miaka ya 2000.

baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo ni kuwa ukimwoana mtu mzima analia mbele za watu ujue kuna jambo.

Kwa kawaida mtu mzima ni mvumilivu, na staahimilivu, hivyo unapoona analia mbele za watu bila aibu yoyote, basi ujue kuna jambo kubwa sana. Inabidi watu wakae chini na kutafuta ni kitu gani kinamsibu ili kukipatia ufumbuzi kwa sababu si kawaida mtu mzima kulia kwenye kila jambo linalompata.

Halafu kwenye miaka ya 1970, kulikuwa na wimbo maarufu uliombwa na Hayati Ahmed Kipande unaitwa 'Kifo cha Penzi.' Anasema kifo cha penzi ni kibaya sana usikiombee, ni heri ufe kwa kugongwa na gari ya tela liendalo Zambia.

Ni wimbo uliokuwa ukielezea mazingira ya zamani yalivyo, kwani kulikuwa na malori ya tela ya kampuni ya Tanzania Zambia Road Service yaliyokuwa yakipakia mizigo bandari ya Dar es Salaam na kuipeleka Zambia. Watoto wa miaka hiyo hata malori yenyewe waliyapachika jina hilo hilo la 'Zambia.'

Kwa jinsi yalivyo, lori na tela lake halafu mwanamuziki anakwambia ni heri kugongwa na lori hilo kuliko kifo cha mapenzi, ni hatari tupu.

Kipande anakwenda mbele zaidi, anakwambia heri kufa kwa kugongwa na basi la ghorofa la kwenda Ilala. Zamani kulikuwa na mabasi ya ghorofa ambayo yalikuwa yakifanya kazi zake Posta, Kariakoo na Ilala tu. Hayakwenda pembezoni mwa mji kutokana na matatizo ya barabara kwani yalikuwa marefu kwenda juu na enzi hizo barabara nyingi bado zilikuwa mbovu.

Sasa kama ni afadhali kufa kwa kupondwa na lori la tela la kwenda Zambia au basi la ghorofa liendalo Ilala kuliko kifo cha penzi, hicho kifo cha penzi ni cha aina gani?

Hapa mwanamuziki huyo anazungumzia maumivu ambayo mtu anayapata pale anapoachana na mke, mume, au mpenzi anayempenda sana.

Fikiria, umewekeza kila kitu kwake halafu mnakuja kuachana kwa tatizo lolote lile, liwe la kwako au lake. Wakati mwingine kuna watu tu wameamua kuliingilia na kulizima kama kibatari au mshumaa.

Moyo unapasuka, unawaka kama moto, unaweza ukiwa unatembea lakini husikii kitu wala huoni. Watu wanaongea huwasikii na gari linaweza kukufungia breki usilione.

Unawaza jinsi mlivyokuwa mnapendana. Mtu ambaye mlikuwa mnabembelezana, mnalishana, mkicheka kwa furaha, leo amegauka kuwa kama adui. Hakupendi tena wala hataki kukuona.

Hii ndiyo tabia ya mapenzi, hayajawahi kuwa na mzani sawa hata siku moja. Ni sawa ni maua tu huchanua na kunyauka. Asubuhi yatachanua na jioni yatanyauka. Ila binadamu yanapochanua hufika kwenye kilele cha furaha na kujisahau kuwa ipo siku yanaweza kunyauka.

Leo tuna wimbo mmoja wa masikitiko uliopigwa na bendi ya Mzinga Troupe iliyokuwa na maskani yake Morogoro. Ni bendi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kama ilivyokuwa kwa Mwenge Jazz. Lakini hii ilikuwa Moro. Ulitungwa na kuimbwa na Hayati Issa Mrisho miaka ya 1980. Unaitwa 'Mazoea Yananikondesha.'

Jamaa alikuwa na mpenzi wake waliopendana sana lakini akatokea mtu fulani akamlaghai binti na akaamua kutoroka naye. Jamaa analalamika sasa, ingawa pamoja na kulalamika kwake hamlalamikii mpenzi wake. Anawalalamikia walimwengu kwa kumchukulia ampendaye. Anasema mpenzi wake hajawahi kuwa na kosa lolote, anaifahamu tabia yake ila amerubuniwa. Mashairi ya wimbo mzima haya hapa:-

"Mazoea yananikondesha eee, nimpendaye kachuliwa mamam aa, wala sina la kutamka wenye nguvu wamenirudia ee, wala sina pa kushtaki wenye nguvu wamenirudia eee.

Tuliishi bila matatizo, nyumbani vitu tele tele wallahi ooo kama mimi nina kasoro wandugu wanata nijulishwe, oooh kwani mmezoea kunichukulia nimpendae.

Daima hakutenda ovu, wala sikutenda ovu, vipi laacha makovu ya kutokusahau milele? Aaah sikutenda ovu la kuweza kulipwa kisasi, wala hakutenda ovu la kutokusahau milele, oooh tuliishi kwa mapendo mama aaah.

Kinachofanya niseme eee, siyo sifa za uzuri wake tu, ama sitopata zaidi yake aa aa, ama nimeshakula kizizi labda, lakini siamini alijua matatizo, kweli nasema mtoto kalelewa.

Kinachofanya nimuwaze eee, siyo sifa ya upole wake tu, ama sifa zake nyinginezo aa aa, hapana alijua matatizo, kwa haki nasema Mungu anjalie.

Walimwengu mama lele, walitaka nitetereke eee. Mbona mjusi ama kinyonga anapata riziki yake, tena hula vijididu hai haswa vyenye kurukaruka, mbona yeye hana mbawa, hana makucha wala vifumbo, hashiki panga wala bunduki, masikini eee, unamtosha ulimi wake, anakula kwa ulimi wake, anapata riziki kwa ulimi wake, sembuse mimi mwanadamu?"

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie kwenu-3

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HAYA ndiyo maisha ya baadhi ya akinamama wa uswahilini haswa wasiopenda kujishughulisha na kazi yoyote, kazi kukaa na kusema ya wenzao, wakati nao wana matatizo mengi tu yaliyowashinda, lakini wala hawayaoni.

Kazi yao akipita mtu anaanza kuchambuliwa ukucha hadi unywele bila yeye kujijua.

Wakati wakimnanga dada mmoja aliyepita dakika moja iliyopita kuwa gauni lake zuri, lakini rangi yake maji ya kunde haikuendana na nguo hiyo, pia ingekuwa ndefu kidogo lakini kaifanya fupi wakati miguu yake mnyembamba kama ufagio wa site, na hata viatu alivyovaa ni fasheni ya kizamani, vimeshapitwa na wakati.

Wakati huo ndiyo James naye alikuwa anapita kutoka kwenye mihangaiko yake akiwa na uchovu kutokana na kazi ngumu alizotoka kuzifanya.

Kinamama na kinadada wakamuacha yule dada, wakaanza kumuongelea kijana wa watu juu ya kilichojiri mtaani hapo siku mbili zilizopita kuwa alimtongoza Carry, lakini vipande alivyopewa hatorudia tena.

"Mtu mwenyewe masikini ya Mungu pangu pakavu halafu anaenda kudandia masista duu."Dada mmoja akachangia mazungumzo ambayo yalionekana kukolea wakimsema mtoto wa watu.

"Mmmh siyo vizuri kumsema mtoto wa watu, mwenyewe hata siyo mkorofi, akituona kama ana hela anatununulia hata karanga, nyinyi mnasema."

Ilikuwa ni sauti ya Sauda. Mtoto mwenye miaka 13 tu ambaye aliwaona akinamama na kinadada wale akiwemo mama yake mzazi ni kama hawamtendei haki James.


Wakashtuka. Halafu mama yake akaongea kwa sauti ya juu, "Tuondoke hapa mtoto wewe, kazi ya umbea tu, watoto wenzako wote hawapo hapa, wako huko wanacheza, wengine wako tuisheni, wewe umejibanza na wakubwa tu hapa ili usikie tunayoongea."

"Siyo hivyo mama, mnamteta mtoto wa watu, vibaya..." Akakatishwa na sauti ya dada mwingine aliyekuwa hapo.

"Unamtetea sana kwani mchumba wako? Mama Sauda na huyu ndiyo anafaa kuolewa naye, akimaliza shule tutamuozesha James."

"Hakuna, mwenyewe hana hata habari na mtu, anacheka na watu wote, huwa anatutetea tukitaka kupigwa njiani, wakati mwingine akituona anatuvusha barabara, mnaniudhi mnavyomsema."

Maneno hayo yalimkera mama yake, akanyanyua kiatu kilichokuwa karibu naye.




Sauda aliliona tukio hilo kabla, akanyanyuka haraka na kukimbia. Wakati mama yake ananyanyua macho alikuwa hatua nyingi kutoka alipo. Akarusha kiatu ambacho kilipita pembeni kidogo.

"Namwambia mwenyewe." Sauda akapaza sauti.

"Wewe wewe Sauda wewe kuwa na adabu nakwambia." Mama Sauda aliishia kulalamika, halafu akamalizia, "watoto wa siku hizi!"

"Nasema kwa mwenyewe." Ilisikika sauti ya Sauda, mwenyewe akiwa haonekani. Alishakata kona kitambo.

"Tuzae tu." mama yake akaishia kusema.

**"Enhee, unataka kunifahamu vipi?" Carry alionekana kutulia ili kumpa nafasi ya kufahamiana. Lakini kwa jinsi alivyokuwa anamwangalia huku akiwa amemshikia kiuno mikono yote miwili ilimuwia vigumu mno James kuongea.**

*******************************

Tukio hili lililokuwa likizungumzwa lilitokea kweli. Lilitokea maeneo ya katikati ya Kinondoni Moscow na Mkwajuni.

Baada ya siku ya kwanza kukutana na Carry na mdogo wake Catty akiwa anatoka kununua mihogo ya kwenda kunywea chai akawasalimia na kumchunia, akitazamwa na Carry kama kinyago, siku nne baadaye James alikutana naye maeneo hayo.

Alikuwa Carry peke yake. Kama kawaida yake, ni mtu mwnye kujiamini na kujaribu licha ya uonekano wake duni.

"Habari yako bibie!" Akasalimia, akiwa tayari kujibiwa lolote lile.

Salamu haikujibiwa haraka. Carry aliyekuwa amevaa blauzi ya nyeupe yenye madoa meusi iliyomkaa vema na sketi ya bluu fupi iliyoacha sehemu ya mapaja yake wazi alimtazama kama mtu ambaye anajaribu kumkumbuka amemuona wapi.

Hata hivyo, bado uangaliaji wenyewe ulikuwa wa dharau.

"Umenisahau dada? Mimi si yule ambaye majuzi tulikutaka kule Kinondoni Moscow chini kidogo hivi? Tena siku hiyo ulikuwa na dada yako." Ilionekana kama Carry kamkumbuka hivi.

"Hivi kwa nini wewe kaka unapenda kutufuatilia, kuna kitu unatudai?"

"Hapana dada."

"Sasa mbona unapenda kutufuatilia mimi na dada yangu, haya siku ile sijui mwenyewe unasema umetusalimia, leo nini tena kimekutuma unisalimie?"

"Dada kwani salamu inagombwa?"

"Wee, koma, aliyekwambia anataka kusalimiwa nani? Kama kusalimiwa mali si ningekuwa nimejaza mapesa ndani."

"Mimi sifanyi hivi kwa ubaya, nataka tu kuwasalimie tufahamiane."

"Enhee, unataka kunifahamu vipi?" Carry alionekana kutulia ili kumpa nafasi ya kufahamiana.

Lakini kwa jinsi alivyokuwa anamwangalia huku akiwa amemshikia kiuno mikono yote miwili ilimuwia vigumu mno James kuongea. Kwa sababu alijua kwa jinsi ilivyo hata akiongea nini sidhani kama atakubaliwa.

"Najua nakuchelewesha." Akaanza kuongea kwa namna ya woga na kigugumizi.

"Ongea vizuri wewe, ningekuwa nachelewa nisingesimama hapa."

"Unajua dada wewe ni mzuri sana, mrembo sana sijaona mwanamke aliyejaaliwa uzuri, aliyeumbwa akaumbika kama wewe katika eneo lote hili kuanzia Kinondoni Mkwajuni hadi Moscow."

"Kwa hiyo, ndiyo unataka kusemaje?" Akauliza kwa dharau akigeuza uso wake kwanza akaangalia sehemu nyingine, halafu akaurudisha kumtazama mzungumzaji kwa namna ya nyodo.

"Niseme tu nimetokea kukupenda Carry."

"We, koma, ishia hapo hapo, kwanza nani kakutajia jina langu?"

"Wewe unajulikana huku kila mtu anakufahamu, kwa nini nisilijue?"

"Kwanza nimekuheshimu wewe kikaragosi, huna hadhi ya kuongea na mimi."

"Inawezekana, lakini naomba unipe hiyo nafasi tafadhali." Bado sauti yake ilikuwa ya mtu asiyejiamini kutokana na kupata upinzani mkali na dharau kutoka kwa Carry.

"Mimi ni mstaarabu na mwema sana, hutojutia kuwa na mimi, nikubalie." Aliendelea kuomba akiwa hamuangalii Carry usoni.

Ghafla kikafuatia kicheko cha kejeli na dharau kutoka kwa Carry. Halafu akamuuliza kwa sauti, "unasema?"

Ile sura ya ukali na hasira usoni mwake ilitoweka na kubakia ya tabasamu ambalo pamoja na kwamba halikuwa halisi, lakini lilimfanya kuvutia na kuzidi kuonekana mrembo.

"Naomba uwe mpenzi wangu." Akajibu James.

"Naomba uwe mpenzi wangu." Carry akarudia neno hilo kwa namna ya kejeli huku akiwa amebana pua moja kwa kidole.

Wakati huo uso wake aliugeuza na kuangalia sehemu nyingine, alipomaliza kumuiga, akamshikia tena kiuno na kutazama usoni.

"Hivi kama nikikukubalia kikaragosi wewe, utanipa nini? Hivi unavyojiona." Akanyamaza lakini kidole chake akawa anakionyesha kwa James akikishusha na kukipandisha kiasi cha mara nne hivi.

"Umeniona mimi nilivyo? Hivi unaweza kunihudumia ikiwa wewe mwenyewe tu huwezi kujihudumia hapo ulipo.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# DIAMOND, KIBA WAONGOZA KITITA CHA MIRABAHA

**Na Saada Akida**

SERIKALI kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imewataka watumiaji wa kazi za sanaa kulipa malimbikizo wanayodaiwa ili wasanii wapate manufaa kupitia kazi zao.

Kauli hiyo imetolewa juzi jijini Dar es Salaam, na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Balozi Dk. Pindi Chana, katika halfa ya utoaji wa mirabaha kwa wasanii .

Waziri alisema watumiaji wote wa kazi za sanaa ambao wamelimbikiza malipo yao wanatakiwa kulipa kwa wakati ili wasanii wapate faida kupitia muziki huo.

"Serikali itaendelea kuchukua hatua za kisheria watu ambao wanachukua kazi za wasanii bila sheria, Nitoe wito kwa watumiaji wote wa kazi za sanaa kulipa madeni kwa wale wenye malimbikizo ili wasanii wapate manufaa kupitia, "alisema Waziri huyo.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hamisi Mwinjuma maarufu 'Mwana FA' alipongeza kampuni ya The Tanzania Music Rights Society (Tarmiso) kwa kukidhi vigezo vya kupata leseni ya kukusanya mirabaha ya wasanii nchini.

"Nina imani ukusanyaji utafanyika vizuri kwa haki ili msipokonywe leseni na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Kulikuwa na malalamiko ya wasanii juu ya kutopata haki zao kupitia digital plantform nilitoa mwongozo Cosota na Baraza la Sanaa Taifa 'BASATA' kwa muda wa siku saba, "alisema Mwana FA

Rais wa Shirikisho la muziki Tanzania, Addo Novemba, alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amewekezaji katika sekta hiyo kwa kutoa mikopo kwa wasanii na kuhakikisha wanapata mirabaha kupitia kazi zao.

"Utaratibu uliopo sasa hadi wapigaji muziki ambao wapo nyuma ya wimbo na waandaji wanapata mirabaha ili kukuza uchumi wa nchi unakua kwa pamoja, "alisema Novemba.

Baadhi ya wasanii walipata mirabaha kwa upande wa bongo fleva waliongoza ni Nassib Abdul 'Diamond' aliopata sh. milioni saba laki Saba, wakati Ali Kiba amechukua sh. milioni tano.

Kwa wanawake Zuhura Othman 'Zuchu' amepata sh. milioni 4 na laki saba huku Faustina Mfinanga 'Nandy' apatiwa mgao wa mirabaha sh. milioni tatu na laki tano wakati Maua Sama sh. milioni mbili na laki nne.

Pamoja na wasanii wa bongo fleva lakini waimbaji wa muziki wa hip hop walipata akiwemo Rashid Shaban maarufu Young Lunya alipata sh. milioni moja na laki sita huku G Nako sh. milioni moja na laki mbili.

Muziki wa injili Christina Shusho sh. milioni moja na laki sita huku Rose Muhando sh. milioni moja na laki tano na Good luck Gozbert sh. milioni mbili na laki mbili.

Bendi ya Msongo Ngoma awalipata sh. milioni mbili na laki tatu na Sikinde sh. milioni moja na laki tano wakati Mzee Yusuph upande wa taarab amepata sh. laki tisa.

# *Jitu Baya aingia kambini kuandaa video*

MWANAMUZIKI mkali wa Hop hop nchini, Jitu Baya, yuko mbioni kuachia video ya singo yake mpya 'Wao' hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe, Jitu baya amesema taratibu ya uchukuaji picha unafikia hatua ya mwisho na wakati wowote atakuwa na kazi ngumu ya kutengeneza video ambayo ameeleza itakuwa tofauti na miaka ya nyuma.

"Bajeti ya kuteneneza video iko tayari kinachofanyika kwa sasa ni kutafuta maeneo yatakayotumika ili iwe tofauti na miaka ya nyuma. Nataka kuonyesha mapinduzi ya muziki huu wa Hip hop hapa nchini," amesema Jitu Baya.

Mwimbaji huyo wa kibao cha Mjini, ameendelea kufanya vyema katika muziki huo kwa kutoa nyimbo kali zinazowapagawisha mashabiki wa muziki.



MSANII anayechupukia katika Bongo Fleva kutoka

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**BAYERN WAMTAKA FABINHO**
MABINGWA wa Ujerumani, Bayern Munich wanavutiwa na kiungo wa kati wa Liverpool na Brazil, Fabinho mwenye umri wa miaka 29, ikiwa uhamisho wake wa kwenda Al-Ittihad hautafanikiwa. (*Sky Germany*)

**KANE APANDIWA DAU**
KLABU ya Bayern Munich imepanga kutoa ofa ya tatu kwa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, na wana uhakika wa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. (*Times*)

**ATALANTA YAIBANIA UNITED-**
KLABU ya Atalanta haiko tayari kukubali ya pauni milioni 86 kwa mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund mwenye umri wa miaka 20, ambaye analengwa zaidi na Manchester United. (*Mail*)

**AMRABAT BADO SOKONI**
KLABU ya Fiorentina inasema bado hawajapokea ofa rasmi kutoka kwa Manchester United kwa ajili ya kiungo wake raia wa Morocco, Sofyan Amrabat, mwenye umri wa miaka 26. (*Metro*)

**WALKER AITAKA BAYERN**
MLINZI wa England, Kyle Walker, mwenye umri wa miaka 33 anatamani kuzungumza na Bayern Munich anapofikiria kuondoka Manchester City msimu huu wa joto. (*Sky Sports*)

**PALACE: TUNAMWAMINI ZAHA**
KLABU ya Crystal Palace ina imani mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 30 atasaini mkataba mpya licha ya kutakiwa na Al-Ettifaq na Lazio. (*Telegraph*)

**CITY YAMSHINIKIZA SILVA**
KLABU ya Manchester City wanamshinikiza kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva, mwenye umri wa 28, kujibu kuhusu ofa yao mpya ya mkataba wa kumlipa mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki. (*Mirror*)

**FOREST YASAKA WAPYA**
KLABU ya Nottingham Forest inajaribu kusajili wachezaji wawili kutoka Manchester United, winga wa Sweden, Anthony Elanga mwenye umri wa miaka 21, kwa mkataba wa kudumu na mlinda lango wa England, Dean Henderson (26), kwa mkopo. (*Fabrizio Romano*)

**WAHI AKARIBIA ATLETICO**
KLABU ya Atletico Madrid wanajiandaa kushindana na Chelsea kumnunua mshambuliaji wa Montpellier, Elye Wahi, mwenye umri wa miaka 20. (*Express*)

**TELLES ANUKIA SAUDIA**
MLINZI wa kushoto wa Brazil, Alex Telles, mwenye umri wa miaka 30 yuko mbioni kukamilisha uhamisho wake wa pauni milioni nne kutoka Manchester United na kwenda Al-Nassr. (*Mirror*)

**AINA KUSAJILIWA FOREST**
KLABU ya Nottingham Forest pia inakaribia kumsaini mchezaji huru, Ola Aina, mwenye umri wa miaka 26, baada ya mkataba wa beki huyo wa Nigeria kukamilika Torino.(*Nottingham Post*)

**LIVRAMENTO MAMBO SAFI**
MLINZI wa kulia wa Southampton na Timu ya Taifa ya England ya vijana wa umri chini ya miaka 21, Tino Livramento, anakaribia kuhamia Newcastle United. (*Chronicle Live*)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AFUNGA BAO LA KWANZA MIAMI

**●●● Mashabiki wampokea kwa shangwe nyota huyo wa soka kutoka...**

**MIAMI,** Marekani

LIONEL Messi alianza maisha yake katika Klabu ya Inter Miami kwa kishindo huku 'mchawi' huyo wa Argentina kwenye mchezo wake wa kwanza akifunga bao la ushindi kwa mkwaju wa faulo dhidi ya Cruz Azul, dakika za lala salama, juzi.

**Miezi saba baada ya kubeba Kombe la Dunia, macho ya walimwengu wa soka yalielekea Florida huku mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or alipoonekana kwa mara ya kwanza kwenye soka la Marekani.**

Baada ya bao bora la kwanza la Robert Taylor na likasawazishwa na Uriel Antuna, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alifunga bao la ushindi katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa DRV PNK na kuifanya timu yake kuondoka kifua mbele kwa magoli 2-1.

Ilikuwa mwisho wa ndoto ya jioni ambayo ilivutia mashabiki wa kila rika wakiwa wamevalia jezi iliyoandikwa 'Messi 10', wakiwa na nyota mpira wa kikapu kama LeBron James, nyota wa tenisi, Serena Williams, Kim Kardashian na David Beckham, miongoni mwa wale waliokuwa kwenye umati uliojaza uwanja.

Inter walianza kwa kuchukua uongozi muda mfupi kabla ya mapumziko kwa bao la Taylor.

Fowadi huyo alishangiliwa kwa muda wote na alipokelewa kwa shangwe kubwa na mashabiki waliojaa uwanjani hapo.

Jordi Alba pia amesajiliwa kujiunga na kocha wao wa zamani wa Barcelona, Tata Martino huko Miami, lakini bado kuna kazi ya kufanya na hilo lilikuwa wazi kwani Azul alistahili kusawazisha kupitia Antuna.

Huu ulikuwa wakati mzuri sana kwa Ligi Kuu Marekani na usiku muhimu kwa soka la Marekani Kaskazini, miaka 48 baada ya Pele kuichezea New York Cosmos na miaka 16 tangu Beckham aanze kuichezea LA Galaxy kwa mara ya kwanza.

## Partey atakiwa kubakia Arsenal

**NEW JERSEY,** Marekani

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, ana imani, Thomas Partey, atabakia Emirates, licha ya kuwasili kwa nyota wa England, Declan Rice.

Kiungo huyo wa kati wa Ghana amekuwa akihusishwa na kuhamia Al-Ahli ya Saudi Arabia, lakini Arteta alisema bado yeye ni sehemu muhimu ya mipango yake.

Akizungumza kabla ya mechi ya jana kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Manchester United huko New Jersey Marekani, Arteta alisema: “Bila shaka, Thomas Partey ni mchezaji muhimu sana kwetu na kwangu. Nataka awe kwenye timu.


“Kila nilipozungumza naye na kila ninapokuwa na mazungumzo naye mapenzi yake ni kukaa nasi. Kwangu mimi.”

Alisema kuwasili kwa Rice haimaanishi kupunguzwa kwa jukumu la Partey.

“Wanaweza kucheza pamoja na hiyo ilikuwa katika mipango yangu,” alisema. “Unataka kuboresha kikosi na kuwa na ubora zaidi.

“Tunahitaji wachezaji ambao wanaweza kucheza pamoja, lakini tunahitaji wachezaji walio katika nafasi moja ambao wanaweza kupigania nafasi zao.

“Ni kitu ambacho hatujapata kwa miaka michache iliyopita na tulitaka kuboresha hilo na ndiyo sababu tulimnunua Declan.”






## PSG YAMWACHA MBAPPE KATIKA ZIARA YA JAPAN

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappé ameondolewa katika kikosi cha Paris Saint-Germain kilichosafiri jana kwenda Japan kwenye ziara ya kujiandaa na msimu mpya, na vyanzo vimeiambia ESPN mabingwa hao wa Ufaransa wanafikiria kutomchezesha tena nyota huyo.

Mbappé mwenye umri wa miaka 24 amebakiwa na mwaka mmoja pekee katika mkataba wake na ameiambia klabu hiyo ana nia ya kumaliza mkataba wake na kuondoka kama mchezaji huru msimu wa joto wa 2024.

Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, hapo awali alisema Mbappé lazima asaini mkataba mpya msimu huu ili kusalia katika klabu hiyo au aamue kuondoka sasa, kwa sababu hawapo tayari kumwacha aondoke bure.

Vyanzo viliiambia ESPN Mbappé, ambaye aliambiwa habari hiyo Ijumaa baada ya kufunga bao katika ushindi wa 2-0 kwenye mechi kirafiki dhidi ya Le Havre, alishangazwa na hatua hiyo lakini ameikubali.

“Wachezaji ambao hawataki kuwa hapa, mlango uko wazi,” alisema Al-Khelaifi akikiambia kikosi hicho hapo Jumanne bila kumtaja mwanasoka huyo wa Ufaransa ambaye alikuwapo chumbani.

Hata hivyo, Mbappé hatabadili mawazo yake na kusaini mkataba mpya. Alirudia msimamo huo kwa mara nyingine kwa klabu mapema wiki hii, jambo ambalo lilimkasirisha zaidi Al-Khelaifi.

Mbappé, ambaye alimaliza kama mfungaji bora wa Ligue 1 katika misimu mitano iliyopita, alituma barua kwa PSG mwezi uliopita akieleza hana nia ya kuongeza mkataba wake.

Lakini baadaye alifafanua hakuiomba klabu hiyo ya Ufaransa imruhusu kuhamia kwa miamba ya Hispania, Real Madrid, ambayo siku za nyuma ilijaribu na kushindwa kumpata nyota huyo.

ESPN iliripoti wababe hao wa LaLiga wana kila kitu kikiwa tayari watakapopata taa ya kijani kutoka kwa Mbappé au PSG. Wanafahamu mpango huo utazidi euro milioni 200 kutokana na ada, nyongeza na kamisheni.

Madrid ndio klabu pekee ambayo Mbappé anataka kujiunga nayo msimu huu wa joto, vyanzo viliiambia ESPN, na ndio timu pekee inayoweza kumnunua.

Kulingana na vyanzo vya ESPN, hakujakuwa na mawasiliano kati ya klabu hizo mbili, lakini Madrid wamekuwa wakizungumza na wawakilishi wa Mbappé kwa muda.

# Sterling: Lishe tofauti iliniathiri

**LONDON,** England

RAHEEM Sterling amesema mabadiliko ya mlo yaliathiri msimu wake wa kwanza Chelsea na huenda yalichangia matatizo ya utimamu wa mwili.

Fowadi huyo alicheza mechi 38 katika michuano yote akiwa na Chelsea baada ya kujiunga akitokea Manchester City kwa uhamisho wa pauni milioni 47.5 Julai, mwaka jana, lakini alipata matatizo ya mara kwa mara ya misuli ya paja na kutemwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England.

Sterling alikaa nje ya mechi ya kufuzu kwa Euro 2024 dhidi ya Malta na Macedonia Kaskazini iliyochezwa Juni, mwaka huu, kufuatia mazungumzo na Kocha wa England, Gareth Southgate, ambaye baadaye alisema winga huyo “hajawa fiti fiti kimwili na hali yake.”

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alitatiziza kuwa katika kiwango chake bora mara kwa mara pale Stamford Bridge, lakini analenga kuweka kampeni tofauti nyuma yake kama sehemu ya kikosi cha wachezaji 29 cha Chelsea kwenye ziara nchini Marekani.

Akizungumza kabla ya mechi ya jana ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu England dhidi ya Brighton huko Philadelphia, aliwaambia waandishi wa habari: “Katika msimu nilibadilisha lishe yangu na kwenda kufanya kitu tofauti kidogo ambacho sikuwa nimefanya hapo awali.

“Na sikuwa sawa na hali yangu. Nafikiri pengine kubeba uzito kidogo wa ziada, nilikuwa na matatizo machache ya misuli ya paja na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

“Kuelekea mwisho wa msimu misuli ya paja haikuwa sawa tena. Mimi na kocha tulifanya uamuzi pamoja kwamba jambo bora kwangu kufanya ni kujiuguza ili nipone vizuri.”



# SERIKALI YAKABIDHI MIRABAHA IKISISITIZA KUONGEZA UBUNIFU

**Na Saada Akida**

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imewataka watumiaji mbalimbali wa kazi za sanaa nchini kulipa malimbikizo ya fedha wanazodaiwa ili wasanii wapate manufaa kupitia sanaa hiyo wanayoifanya, imeelezwa. Kauli hiyo imetolewa jijini, Dar es Salaam juzi na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Balozi Dk. Pindi Chana, katika hafla ya utoaji wa mirabaha kwa wasanii.

Chana alisema watumiaji wote wa kazi za sanaa ambao wamelimbikiza malipo yao wanatakiwa kulipa kwa wakati ili wasanii wapate faida kupitia muziki huo.

"Serikali itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa watu ambao wanachukua kazi za wasanii bila sheria, nitoe wito kwa watumiaji wote wa kazi za sanaa kulipa madeni na malimbikizo ili wasanii wanufaike, "alisema Chana.

Naye Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hamisi Mwinjuma maarufu 'Mwana FA' aliipongeza Kampuni ya The Tanzania Music Rights Society (TARMISO) kwa kukidhi vigezo vya kupata leseni ya kukusanya mirabaha ya wasanii hapa nchini.

"Nina imani ukusanyaji utafanyika vizuri na kwa haki ili msipokonywe leseni na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), kulikuwa na malalamiko ya wasanii juu ya kutopata haki zao kupitia digital platform, nilitoa mwongozo kwa Cosota na Baraza la Sanaa Taifa (BASATA)," alisema Mwana FA.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa COSOTA, Doreen Sinare, alisema jumla ya Sh. milioni 326 zimetolewa kwa wasanii katika mchakato huo wa mirabaha.

"Nitoe wito kwa makampuni kujitokeza kujisajili ili wapate leseni ya utoaji wa mirabaha, sisi kama COSOTA tutabaki kama wasimamizi, " Sinare alisema.

Rais wa Tarmiso, Hermes Bariki 'Hermy B' alisema jana wanatambua umuhimu wa mirabaha hivyo anawasihi wasanii wake wabunifu katika kazi zao ili kukuza sanaa kwa kiwango kikubwa.

"Tupo pamoja kuleta maendeleo ya muziki nchini Tanzania, wasanii waongeze bidii katika kazi zao, " Hermy B alisema.

Baadhi ya wasanii walipata mirabaha kwa upande wa bongo fleva ni Nassib Abdul 'Diamond Platnumz' aliyepata Sh. milioni 7.7, Ali Kiba Sh. milioni tano, Zuchu Sh. milioni nne, Nandy Sh. milioni 3.5 wakati Maua Sama amepata Sh. milioni 2.4



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Balozi Dk. Pindi Chana (kushoto), akifurahi baada ya kumkabidhi funguo ya zawadi la gari alilokabidhiwa Miss Tanzania 2023, Tracy Nabukeera. Mrembo huyo aliibuka mshindi katika shindano lililofanyika Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba SC yatambia faida za Miquissone

INATOKA UK. 24

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya 'fununu' za muda mrefu, sasa wamefanikiwa kumnasa nyota huyo kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kikosi chao.

Ahmed alisema kurejea kwa Miquissone ni faida kwa Simba kwa sababu ana uzoefu mkubwa katika mashindano ya Afrika na pia analifahamu vyema soka la Tanzania kutokana na kucheza kwa mafanikio katika kipindi kifupi kilichopita.

"Tayari Miquissone ameshawasili Tanzania kwa ajili ya maandalizi ya safari ya kwenda Uturuki, muda wowote kuanzia sasa ataungana na wachezaji wengine ili kujiandaa na msimu mpya wa mashindano yaliyopo mbele yetu," alisema Ahmed.

Aliweka wazi bado Simba haijamaliza mchakato wa usajili na lengo ni kutaka kutekeleza mapendekezo yote yaliyotolewa na benchi la ufundi kwa ajili ya kufikia malengo ya klabu katika msimu mpya.

Usajili wa Miquissone unaleta mashaka juu ya hatima ya nyota wawili wa kigeni wa timu hiyo, Pape Sakho, ambaye bado hajajiunga na kikosi cha Wekundu hao wa Msimbazi akiwa kwao Senegal na tetesi zikisema klabu moja ya Ubelgiji inamhitaji.

Nyota mwingine ambaye naye yuko katika sintofahamu ni Banda ambaye alikuwa anavaa jezi namba 11 ambayo tayari amepewa Miquissone.

Wakala wa Banda, Tigana Amadou, aliliambia gazeti hili hivi sasa anaendelea na mchakato wa kumtafutia timu nyingine mchezaji wake baada ya kutokuwa na msimu mzuri ndani ya Simba.

Amadou alisema baada ya Banda kupoteza namba katika kikosi cha kwanza, hali imekuwa nguvu kwake na wamefikia uamuzi wa kutafuta timu nyingine ili akajaribu changamoto mpya.

"Bado naamini Banda ni mchezaji mzuri, lakini msimu uliopita alishindwa kuwa katika kiwango kizuri baada ya kuandamwa na majeraha yaliyomfanya akae nje kwa muda mrefu.

Tunaendelea kupambana kutafuta timu ambayo itampa nafasi ya kucheza zaidi ili aweze kurejea katika kiwango chake kama ilivyokuwa awali," alisema Amadou.

## Skudu, Mkude waiteka Yanga

INATOKA UK. 24

buiza katika tamasha hilo ni Mzee wa Bwax, Christian Bella, Mavocali, Sharo Mwamba, Dullah Makabila, Marioo na Rayvany aliyeingia na 'kijiji'.

Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Raymond Shaaban, ameingia uwanjani na madensa wasiopungua 100 ambapo walizunguka Uwanja mzima, aliimba nyimbo tatu ikiwamo wimbo maalum wa Yanga ambao amewasifia viongozi wa klabu hiyo.

Mapema mchana, kikosi cha Yanga Princess kilianza vyema msimu kwa kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya timu mpta iliyopanda daraja, Geita Gold Queens kutoka mkoani Geita wakati mchezo mwingine uliowakutanisha wafanyakazi wa klabu hiyo ya Jangwani dhidi ya wasanii ulimalizika kwa sare ya bila kufungana. Baada ya tamasha hilo kumalizika, mabingwa hao watetezi wataendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Singida Fountain Gate FC.

Yanga ambayo msimu uliopita ilicheza fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, pia ndio mabingwa watetezi wa Kombe la FA na Ngao ya Jamii.

Kabla ya mechi kuanza jana, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema amefurahishwa sana na mapokezi ambayo amepewa na hakuamini kile alichokiona.

"Nina furaha sana, nimefurahia sana haya mapokezi, nimefurahi kuwa sehemu ya kikosi hiki," Gamondi alisema.

## *Prisons kusajili wachezaji sita*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushindwa kwenda Zanzibar kama ilivyotarajiwa, kikosi cha Prisons kinajiandaa kuelekea Musoma, mkoani Mara ili kuweka kambi ya kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa 2023/2024 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Prisons pia itashiriki mashindano ya kuwania Kombe la FA ambayo bingwa wake ataiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kocha Msaidizi wa Prisons, Shaaban Mtupa, alisema kikosi chao kinaendelea vyema na mazoezi yake jijini, Mbeya wakati wowote wataelekea Musoma ili kwenda kukamilisha programu ya 'pre season'.

"Maandalizi yetu yanakwenda vizuri hapa Mbeya, kikubwa tunajiandaa na ligi kwa sababu tunajua itakuwa ngumu kuliko iliyopita, kuhusu tutakapoelekea kuweka pre season," alisema Mtupa.

Kuhusu usajili, kiongozi huyo alisema wanajiandaa kusajili wachezaji wapya sita ambao watakiongezea nguvu kikosi chao ili kukabiliana na ushindani utakaokuwapo.

Alimtaja straika, Salum Kihimbwa, tayari wameshamsajili na wamemnasa akitokea Mbeya City.

Kabla ya kutua Mbeya City, Kihimbwa aliichezea kwa muda mrefu Mtibwa Sugar.

# Michezo

Jumapili Julai 23, 2023

Nipashe




UK. 22

## PSG yamwacha Mbappe Japan



# SKUDU, MKUDE WAITEKA YANGA

## Gamondi afunguka amefurahishwa mapokezi makubwa ambayo kwake...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

RASMI mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wametambulisha kikosi chao cha msimu wa 2023/2024 huku wachezaji wawili wapya, Mahletse Makudubela 'Skudu' kutoka Afrika Kusini na kiungo Mtanzania, Jonas Mkude, wakishangiliwa zaidi.

Mashabiki wa Yanga walifika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana walionyesha mahaba kwa wachezaji hao, ikiwa ni ishara wanatarajia makubwa kutoka kwao kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Majina ya wachezaji hao yalikuwa ya mwisho kutambulishwa baada ya kuitwa Mkude aliyeachwa na Simba, mashabiki walinyanyuka na kushangilia kwa kuwapa heshima kutokana na ujio wao.

Skudu, ulikuwa ni utambulusho wa mwisho na aliingia kwa mbwembwe kwa kucheza muziki wa staili ya Mapiano na kuchezea mpira ambao uliishia mikononi kwa kipa chaguo la kwanza wa timu hiyo, Djigui Diarra, ambaye naye alishangiliwa kwa kuonyesha umahiri wake wa kudaka.

Katika orodha ya majina 26 ya wachezaji wa Yanga msimu huu mpya wa Ligi Kuu Tanzania inaotarajia kuanza Agosti 15, 2023, jina la Yannick Bangala na Shaban Djuma hayako katika majina yaliyotajwa katika utambulisho huo.

Pia kati ya wachezaji hao waliotambulishwa jana, 17 ni nyota wa zamani, saba wapya, watano wa kigeni na wawili wakiwa ni wazawa.

Utambulisho wa kwanza ulikuwa saa 11:22, Bakari Mwamnyeto akifungua dimba la utambulisho huo akiwa amevalia jezi yake namba tatu ambayo alikuwa akitumia msimu uliopita, na baada ya hapo ikafuata zamu ya makipa wote watatu akiwamo Diarra (39), Abdultwalib Msheri (16) na Metacha Mnata (1), wachezaji wengine ni Denis Nkane ambaye amebadilisha jezi na sasa anatumia jezi (40) ambayo awali alikuwa akivaa Clement Mzize atakayetumia (24).

Wengine ni Farid Mussa (17), Joyce Lomalisa (13), Jesus Moloko (12), Ibrahim Bacca (2), Chrispin Ngushi (11), Mudathir Yahya (27), Stephen Aziz Ki (10), Khalid Aucho (8), Salum Aboubakar 'Sure Boy' (18), Dickson Job (5), Zawadi Mauya (20), Kennedy Musonda (25), Pacome Zouzoua (26) na Nickson Kibabage (30).

Beki Kibwana Shomari sasa atavaa jezi namba 33 ambayo msimu uliopita ilivaliwa na Bernard Morrison, Max Nzengeli (7), Gift Freddy (37) na Kouassi Yao atavaa jezi namba (21) iliyokuwa inavaliwa na Djuma.

Mbali na kuonyesha uwezo wake wa kucheza kabumbu, nyota mpya wa Yanga, Mahletse Makudubela 'Skudu' alishindwa kuvumilia kwa kuamua kucheza Mapiano wakati akitambulishwa rasmi mbele ya mashabiki kuwa ni mmoja wa wachezaji timu hiyo.

Kama haitoshi, Skudu tena aliamua kuambatana na Juma Jux, kucheza kibao maarufu msanii huyo wa bongo flava kinachotamba sasa kiitwacho 'Huyu Demu Wake Nani' huku wachezaji wenzake wakiwa wamerejea vyumbani tayari kujiandaa na mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Kaizer Chiefs kutoka Afrika Kusini.

Wasanii wengine waliotum-

INAENDELEA UK. 23

## Simba SC yatambia faida za Miquissone

**Na Saada Akida**

HATIMAYE winga wa Timu ya Taifa ya Msumbiji, Luis Miquissone (27), amerejea rasmi kwa Wekundu wa Msimbazi kwa kupewa mkataba wa miaka miwili, imeelezwa jijini, Dar es Salaam jana.

Miquissone amerejea Tanzania baada ya kufikia makubaliano ya kuvunja mkataba na vigogo wa Afrika, Al Ahly ya Misri, ambayo ilimsajili akitokea Simba.

Mchezaji huyo hakuwa na msimu mzuri na Waarabu hao katika kipindi chote alichokaa Misri.

Taarifa zilizopatikana kutoka katika klabu hiyo zinasema Miquissone atakabiziwa jezi yenye namba 11 mgongoni ambayo msimu uliomalizika ilikuwa ikivaliwa na mshambuliaji, Peter Banda.

Winga alikuwa akivaa jezi yenye namba hiyo alipokuwa akiitumikia Simba hapo awali.

Akizungumza na Nipashe jana,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >